

IMANI KAMILIFU



Baba yetu uliye Mbinguni, hilo ndilo kusudi letu usiku wa leo. Tumekusanyika pamoja tupate kuamini tu, kumwamini tu Bwana Yesu. Kuna wale hapa, usiku wa leo, walio wagonjwa na wanaoteseka, nasi tumeitoa ibada ye—ye—yetu usiku wa leo kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa na waliovunjika mwili. Sasa, kama mwimbaji alivyoimba huo wimbo mzuri, *Kisha Yesu Akaja*, na ujitokeze kwetu usiku huu, Bwana, na ukawaponye wote walioteseka, na hakutakuwako na mtu aliye mnyonge miongoni mwetu usiku wa leo. Tujalie, Bwana, na utusaidie tunapolitazamia Neno sasa kupata imani inayotosheleza kwa ajili ya majira haya. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

² [Ndugu Branham ananena na mtu fulani jukwaani—Mh.] Kuna miwani hapa, ambayo mtu amepoteza, nayo ikapatikana kanisani. Iwapo mtu ye yote... ikiwa ni yako, vema, iko hapa jukwaani, mimbarani.

³ Naam, najua ya kwamba wengi wanafanya kazi, na hawana budi kwenda nyumbani mapema, na kwa hivyo sitazungumza muda mrefu; kisha tuna mstari wa maombi kuomba wagonjwa. Hiyo inanipa nafasi ku—kushughulikia walio hatarini ambao wameletwa hivi sasa chumbani, nimewaangalio sasa hivi nilipokuwa nikija, pia adhuhuri ya leo. Wengine wao, bila shaka, ni wagonjwa sana na ni wakali sana. Na wamekuwa wakipiga simu kuwaomba wagonjwa. Kuona mkono wa Bwana Yesu ukiwaponya wagonjwa na wanaoteseka, ni wa ajabu vipi!

⁴ Sasa, si mara nyingi sana tunapofanya hizi ibada za uponyaji, kwa maana kwa kawaida sisi... Roho Mtakatifu atajitokeza iwapo mna kisa cha hatari, na kukitambua upesi sana, na kukiteua na kusema jambo fulani kukihusu. Kisha waliobakia, naam, tuna... labda si wabaya sana, kwa hivyo tunawapita tu. Nami nalidhani, tukiwa humu mara mbili kwa siku, inafaa tutenge ibada moja kwa ajili ya kuwaomba wagonjwa. Naamini katika kuwaomba wagonjwa. Naamini ni amri ya Biblia. Hatuwezi kuhubiri hayo, bila... Injili yote, bila kuwa na hayo.

⁵ Sasa, inawezekana... sijui bado, sijapiga simu nyumbani bado, usiku wa leo, huenda ikawa Jumapili ijayo nitapitia hapa tena. Na iwapo—iwapo hamtasikia kutoka kwetu, iwapo Billy hatawaarifu (atajua baadaye kidogo katika juma hili), msiposikia, basi tutakuwa hapa Jumapili ijayo; maana hiyo inawapa siku ya Wafanyi Kazi, mwaona, kupumzika, na hivyo basi... ama kurudi nyumbani. Mwaona? Na kwa hivyo tutajaribu, Bwana akipenda. Sasa, vema, msiposikia... nafikiri Billy huwatumia kadi, ama huwaarifu kwenye ibada kwa njia

fulani, kwa hivyo asipowapigieni simu, basi ninarudi kwa—kwa. . . Jumapili hii ijayo. Ndugu Neville, ikiwa ni sawa kurudi? [Ndugu Neville anamzungumzia Ndugu Branham—Mh.] Lo, hiyo ni sawa.

⁶ Ye yote anayetaka kujua, huyo mtoto wa Collins, hapa. Na katika wakati wa zile Mihuri Saba, daktari alikuwa amemwambia huyo kijana, mwenye baridi yabisi, ya kwamba ilimpasa kulala chali na kunywa akitumia mrija; ndi—ndivyo ilivyokuwa. Na baba na mama wakamleta nyumbani na kumketisha chumbani, nikamwombea. Na Bwana Yesu akamponya kabisa, akarudi shuleni; nao wenye mamlaka wakawapigia simu kuhusu hayo. Kwa hivyo wakamwita mtaalam aliyekuwa akimtibu, naye hangaliamini—hangaliamini kitu kama hicho, nao wakamleta huyo mvulana wapate kumfanyia uchunguzi. Naye alikuwa hajambo kabisa, mzima kama kawaida. Kisha, Yesu akaja, nguvu za mjaribu zikavunjwa!

⁷ Mwajua, ajabu ni kwamba, nilikuwa nimuulize mtu fulani kuimba wimbo huo usiku wa leo. Nami nilipokuwa nikihudumu mle chumbani, ndio huu unakuja, mtu fulani akiuimba mle, *Kisha Yesu Akaja*. Kama huo—huo usingaliimbwa, ningalimuuliza mtu fulani auimbe kabla si—sijanena usiku wa leo. Kwa hivyo, Ye—Yeye hutenda mambo yote vyema.

⁸ Basi wengine wenu watangoja hata asubuhi, walio na safari ndefu, nami na—nathamini hiyo—hiyo juhudi. Wengine wenu wataenda nyumbani kwa motokaa usiku wa leo maana inawabidi kwenda kazini asubuhi na mapema, nami na—najua ni vigumu. Ndiposa ninapowaza, kuona hayo, . . .

⁹ Mimi pia huduwaa, mwajua; hupatwa na moyo mzito. Ninafikia ambapo mimi. . . Inayonishida mimi, ni ambapo mimi huduwaa ninapofanya kazi sana, naye shetani ananijia akiniambia, “Vema, hamna anayekujali. Kwa kweli huna rafiki ulimwenguni, mwaona.” Na ili kwamba. . .

¹⁰ Kumbuka, mimi si asiyepatwa na majaribu. Mwaona, sina budi kuyashinda hayo. Kisha ninapotazama nyuma na kuona jambo kama hili, ninamrudishia usoni mwake na kusema, “Na hiyo je?” Hiyo hunisaidia ku—kushinda. “Na hiyo je?”

¹¹ Kama rafiki fulani wangu, anayeketi m—mkutanoni hapa, kulikuwa na—na—na kundi, kundi fu—fulani ambalo haliamini katika uponyaji wa Kiungu, aliyekuja kwa huyu kijana hivi majuzi akamwambia, “Kitu hicho wanachohubiri pale kuhusu uponyaji wa Kiungu, hamna kitu kwake.”

¹² Na mtu huyu huishi Kentucky, karibu sana na mwanamke kizee ambaye, tulipokuwa kule kwenye kambi ya Akton, alikuwa yuafa kwa kansa. Naye dada yake akaja mkutanoni usiku huo akiwa na lesa kibetini mwake ambayo alikuwa amechukua, naye Roho Mtakatifu akamwita huyo mwanamke nyuma kule (nami

sikuwa nimeenda katika nchi hiyo hapo awali) na kumwambia ya kwamba “Yeye alikuwa na lesa kibetini mwake, alichokuwa nacho, na alichotoa nyumbani, naye dadaye alikuwa juu ya kilima fulani kule, akifa kwa kansa ya tumbo. Daktari amemkatia tamaa.” Nami nikasema, “Nenda kaweke hiyo lesa juu ya huyo mwanamke, maana BWANA ASEMA HIVI, ‘Yeye ataishi.’” Na huo ndio ule usiku, jirani mle walidhani ya kwamba walikuwa na Jeshi la Wokovu, wakati Ndugu Ben alipoenda kule, kisha akaweka . . . Naye huyo bibi aliponywa kabisa hata yeye hufanya kazi yake mwenyewe na kazi ya jirani yake.

¹³ Kwa hivyo huyu kijana mwanamume, akijua hilo, yeye akasema, “Basi eleza kisa chake! Hiyo yatosha. Eleza; unajua yeye alikuwa na kansa. Alikuwa hapa Louisville nao madaktari walimfanyia upasuaji, kisha wakamgeuza tu, ‘mshone, mrudishe, kwa maana haiwezekani kumfanyia cho chote.’ Na sasa yeye ni mzima kabisa, vema.” Kasema, “Eleza hayo.” Hilo latosha. Mwaona?

¹⁴ Unajua Biblia ilisema nini? “Nao hawangelisema lo lote makosa, kwa kuwa huyo mtu alikuwa amesimama kati yao, ambaye kwake ulifanywa huo muujiza.” Hapo ndipo sisi . . . Inamtahayarisha shetani, siyo? Yule mtu alikuwa amesimama pale ambaye alifanyiwa huo muujiza.

¹⁵ Je, Mungu hufufua wafu? Hapa yuaketi mtu, papa hapa, aliyefufuliwa toka kwa wafu. Mungu huponya wagonjwa? Lo, jamani, mikonogeinuliwa kila mahali. Mungu huponya wagonjwa. Nasi tunajua Yeye ndiye MIMI NIKO, aliye m—mkuu, si “Nilikuwa” au “Nitakuwa” aliye Mkuu; MIMI NIKO. MIMI NIKO, hiyo ni “aliyeko daima, kila mahali, wakati wote”; yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁶ Sasa, tupate kuharakisha, hebu sasa tuigeukie Biblia iliyobarikiwa. Nataka kusoma fu—fungu la maneno a—ambalo “likikuwa likinigeuza” nilipolisoma. Nami nataka kuwa na mstari wa maombi usiku wa leo, na kumwomba kila mtu anayetaka kuombewa.

¹⁷ Na sasa tutafungua Marko, Mt. Marko, sura ya 11 ya Marko. Nasi tutaanza kusoma yapata—yapata kifungu cha 22 cha sura ya 11 ya Marko. Na wengi wenu mnajua Andiko hili, limejulikana sana. Ndilo Andiko nililokuwa nikiwazia, Ndugu Russell, wakati hao . . . aliponena nami na kusema habari za hao kuchakulo. Nao . . . hilo ndilo Andiko nililokuwa nikiwazia. Limekuwa fumbo daima. Yeye alisema, “Kama wewe ukisema”; si “kama mimi nikisema”; si “Kama wewe ukisema!”

¹⁸ Sasa, hebu na tusome:

. . . Yesu akajibu, akawaambia, Mwaminini Mungu.

Amini, nawaambia, Ye yote atakayeambia mlima huu, Ng’oka ukatupwe baharini, wala asione shaka

moyoni mwako, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.

Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.

Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni...ili Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.

[Lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.]

¹⁹ Sasa, imani ina msingi wake katika msamaha, basi. Ndiposa, kama tulivyosema asubuhi ya leo, tukijaribu kuliweka kanisa mahali ambapo tungeweza kuona kweli nyakati za kimitume zikitenda kazi miongoni mwetu, hayo ndiyo tunaonea njaa. Na yako mlangoni kabisa. Tunayaona, bali tunataka kuona mengi zaidi. Tunataka kuona wingi wake sana hata i—itatusaidia, kuwapelekea wengine.

²⁰ Kumbukeni, Yesu (kama tulivyoona katika lile somo asubuhi ya leo), Yeye hakutumia Uwezo Wake kwa ajili Yake Binafsi, aliutumia kwa ajili ya wengine. Hilo ndilo kusudi la huo kutumwa. Unadhani wakati mwingine, “Kwa nini mtu aliyekuwa amejazwa uwezo, kama Yeye, ilimpasa kuwa mgonjwa?” Naam, bwana. Nimekwisha soma katika kitabu fulani, mahali fulani alipomfufua yule kijana, yule mwana wa mjane kutoka Naini (naamini, *Yule Mtawala wa Nyumba ya Daudi*), ya kwamba aliketi juu ya mwamba na kuugua kuumwa na kichwa. Waona? Yeye alichukua udhaifu wetu. *Kuchukua* maana yake ni “kuubeba.” Mwaona, akauchukua. Naye alikuwa na mambo yote katika...jinsi tulivyo nayo. Alikuwa na magonjwa, alipata majaribio, alikuwa na shida, alipata pingamizi kama tunavyopata, kwa maana ilimpasa kuwa Mpatanishi anayefaa; kwa hivyo ilimpasa kuwa mshiriki, Mkulima wa matunda, kabla hajajua. Yule mwanamke kisimani na mambo mingi, mnaona, kama tungalitazama moja kwa moja katika Maandiko.

²¹ Nataka kusema ya kwamba naamini kila Andiko, na kila moja kuwa ni kweli. Kuna watoa lawama siku hizi ambao hawataki kuamini hayo. Mtoa makosa siku moja alisema ya kwamba “wakati Yesu aliwatuma hao wanafunzi hata mahali huyo punda alikuwa amefungwa, kwenye njia panda, ya kwamba Yeye alipanga hapo mbeleni ambapo huyo mwana punda angefungwa.” Mnaona, wao hawafahamu ya kwamba *Mungu* alipanga hayo kimbele.

²² Mungu aliniambia, hivi majuzi, na Bwana Dauch hapa, ya kwamba “ningemsalimia kwa mkono, barabarani tena.” Hiyo ni ajabu sana, sikuwa hapa asubuhi hiyo; ila dakika mbili zaidi, ama dakika moja zaidi, singalikutana naye barabarani. Bali

nilitoka tu motokaa ni nipate kumsalimia kwa mkono alipokuwa akija humu, barabarani. Yeye hakunijua; yeye alikuwa ametoa miwani yake, hangaliniona. Aliposikia sauti yangu, akaanza kulia. Ilikuwa nini? Kwa kawaida yeye hafanyi hivyo, bali lilikuwa jibu la yale aliyoarifiwa kule chini ya hema la oksijeni; angefanya hivyo.

23 Nikasema, “Utaketi pia kanisani tena”; hamu ya moyo wake. Tulipokuwa na mkutano wa Chicago, yeye alitaka kuja katika mkutano huo, moyo wake ulitamani hayo. Nalimtumia simu za salamu zetu na watoto, kumwambia ya kwamba tulikuwa tukiomba ya kwamba angepata afya, upesi sana. Na ndugu mpendwa, aliyemtembelea, alisema ya kwamba ali—alitaka tu kuja sana. Bali ndiye huyu ameketi hapa, usiku wa leo, pamoja nasi. Mwaona? Hayo hayakupangwa kimbele. Mungu yule yule aliyapanga, Yeye hufanya kila kitu kufanya kazi kikamilifu na wakati unaofaa kabisa.

24 Mtoa makosa siku moja alisema ya kwamba “Si ajabu Yesu angetwaa mikate mitano na kuwalisha elfu tano,” kasema, “mikate siku hizo ilikuwa mikubwa, naye akakata kata kila mkate kuwalisha elfu moja.”

25 Nataka ufahamu, mvulana mdogo alikuwa nayo kwa ajili ya chakula chake cha mchana! Mtoto mdogo alibeba mikate mitano ambayo ingewalisha elfu tano, na kushiba. Naam, basi, na vile vikapu kumi na viwili vilivyookotwa baadaye? Mwaona? Lo, wao . . . hao ni wapinzani tu, hiyo tu. Hilo halibadilishi Neno la Mungu. Ni jambo lile lile, linaendelea.

26 Sasa tunataka kunena juu ya imani, na imani ya aina tofauti: Imani Kamilifu. Hilo ni jambo kubwa. Basi, imani, tunaambiwa katika Biblia, “*Imani chanzo chake ni kusikia.*” Sasa, huwezi kuokolewa bila imani. Na imani ni kitu ambacho huna budi kuamini ya kwamba kiko, ambacho hamna kingine kinachoweza kukitangaza ila imani. Naam, ninajaribu kuwaletea imani, kusudi mpate kuwa tayari kwa ajili ya mstari huu wa maombi, katika dakika chache zijazo.

27 Sasa, imani: “*Mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko.*” Na haiwezekani ku—kumpendeza Mungu pasipo imani, hauwezi kumpendeza. Na ukisema unamwamini Mungu . . . haujamwona kamwe, waona, kwa hivyo basi huna budi kuamini kwa imani. Na kama ungemwona Yeye, haingekuwa tena imani. Waona? Cho chote ambacho zile hisi hutangaza, si imani tena, ni kweli ya sayansi; waona, na si imani tena. Bali inakubidi umpokee kwa imani. “*Na mtu amwendeaye Mungu lazima aamini ya kwamba Yeye ni Mungu; na imani chanzo chake ni kusikia Neno la Mungu.*” Waona, huna budi kuamini hili ni Neno la Mungu, na huna budi kuja kwa Mungu kwa Neno. Waona? Chukua tu Neno, jinsi lisemavyo, na “Hiyo ni kweli!” Cho chote kinginecho kilicho kinyume chake, si kweli.

²⁸ Ilimbidi Ibrahimu kuamini tu yale ile Sauti ilimwambia. Na alipokuwa na umri wa miaka mia moja, miaka ishirini na mitano baadaye, aliliamini zaidi ya alivyoliamini miaka ishirini na mitano hapo mbeleni ilipotolewa kwake. Unaona? Yeye aliiamini. Na “Hakusita katika ahadi za Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu, akijua ya kwamba Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.” Na hiyo ndiyo njia, kila mtu inampasa kuwa hivyo. Huna budi kuja kwa imani isiyoshindwa, ukiamini ya kwamba Mungu ndiye aliyefanya hiyo ahadi. Bali sasa, inakupasa uwe katika mahali unapoweza kuwa na imani hiyo, na hayo ndiyo tunayonena juu yake unaona, kuipokea imani hiyo.

²⁹ Katika Waebrania, Kitabu cha Waebrania, sura ya 11, tunaambiwa ya kwamba:

*... imani ni kuwa na hakika ya mambo
yatarajiwayo, ...*

³⁰ Basi, hapo ndipo watu wengi hukosa kupokea uponyaji wao, ama kile wanachoomba, kwa sababu wao huchukua imani kuwa kitu isicho. Unaona? Hawaamini. Ni—ni... si—si mawazo. Ni kitu kilichoko hasa.

³¹ Basi, sikizeni kwa makini! Waona, si yale unayowazia. Ni dhahiri kwako kabisa kama tu hisi yo yote mwilini mwako itatangaza kitu cho chote kile. Ni halisi tu kama vile macho yangu yasemavyo, “Hiki ni kipande cha karatasi.” Ni dhahiri tu kama kusema, “ile ni nuru.” Ni dhahiri tu kama kusema, “Napapasa koti langu. “Ni dhahiri tu kama ku—kumsikia yule mtoto mchanga akizungumza pale, ama kufanya kelele. Unaona, dhahiri tu kama kucheza muziki. Ni dhahiri tu kama ninavyoonja cho chote mdomoni mwangu. Ni dhahiri hivyo, isipokuwa tu huwezi kumwonyesha mtu mwingine. Unayo peke yako. Amina! Ni yako. Imani ni *kuwa* na hakika; unaona, si hadithi tu. Kwa hivyo, watu wengi huja . . .

³² Naam, haya ni masomo halisi na yenye kilindi, nami nitayagusia juu juu tu, kisha nanyi myachimbue kindani. Mnaona?

³³ Tazama, ni kitu ambacho unacho; si mawazo, kama ni kweli unayo. Ni dhahiri kwako tu kama kitu cho chote kile kingalikuwa. Ni dhahiri tu kama—kama unavyojua ya kwamba—kwamba unaendesha motokaa. Ni dhahiri sana kama unavyojua ya kwamba unaketi kanisani. Ni dhahiri sana kama vile unavyoisikia sauti yangu. Ni kitu chenyewe, si mawazo, si mwamsho; bali kitu ulicho nacho, nacho kinakujia kwa kusikia Neno la Mungu (na Hilo peke yake.) “Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu.” Hiyo inairudisha ambapo imani yako, basi, si katika mtu fulani. Haimo katika mtu fulani. Haimo katika dhehebu. Haimo katika kundi la watu. Imo katika

Mungu, kwa maana Mungu ni Neno. Imani yako imo katika Mungu!

Imani chanzo chake ni kusikia Neno la Mungu!

³⁴ Kisha Mungu, kwa Neno Lake, . . . Si kwa yale mtu mwingine aliyofanya, mtu mwingine alivyosema, bali kwa yale Neno la Mungu lilivyosema. Yeye alisema, “Neno la kila mtu liwe uongo, na Langu liwe kweli.”

³⁵ Basi, ukimwona mtu mwingine akifanya kwa neno, tendo la Mungu, ahadi ya Mungu; na wengi wao husema, “Naweza kufanya hivyo, pia!” (ni mawazo). Na wanapofanya hivyo, unawaona wameharibikia kule nje mahali fulani. (Haina budi kuwa kitu dhahiri!!!) Sasa, hiyo ni imani isiyodhahiri. Hicho ni kitu ambacho kingekuleta kwenye imani. Ni imani kwa uwezekano, kama vile ungaliniomba mti wa mwaloni, nami nikupe tunda lake. Kwa hali isiyo dhahiri una mti wa mwaloni, bali haujachipuka bado; lakini utakapochipuka, ni mti mwaloni. Na unapowaza ya kwamba Mungu hufanya hili, . . . Bali inapofunuliwa kwako, ni imani basi, Imani Kamilifu ambayo haiwezi kushindwa.

³⁶ Hiyo ndiyo sababu hayo maono ni mu—himu sana kwangu, kwa maana yamethibitishwa kuwa “kweli” kila mara. Waona? Nami najua ya kwamba Yeye aliahidi hayo. Naye aliahidi kwa Neno Lake, na hapa yuaja na kuliahidi kwa ajili ya siku hii. Kwa hivyo, unajua unakosimama, aliposema hivyo. Waona, hiyo hunipa imani, kwa maana Yeye hafanyi cho chote kinyume cha Neno Lake lililoandikwa. Waona? Na iwapo kinapinga Neno, singaliweza kuwa na imani kwake. Inaileta moja kwa moja tena kwa Neno (waona?), imani katika kusikia Neno la Mungu. Huna budi kusikia Neno! Neno la Mungu ndilo Neno linalotosheleza kabisa. Unachokihitaji chote, ni Neno hili.

³⁷ Sasa, imani ikiwa hakika ya mambo, na mle ndani tunaona (katika Waebrania) imani ilikuwa nini, na yale hao waliyofanya waliokuwa na imani. Mnaona, kuna wakati mwingi ambapo watu wana imani leo, na kesho hawana; siku inayofuata mna *kitu fulani*, na *kitu kingine*. Bali mara Mungu anapoitia nanga, nawe unaiona, hamna kitu kitakachokufanya utoke kwake. Unapapasa tu, unafikia, unathubutu (na *kuthubutu* ni “kufanya pasipo ruhusa”); unajaribu tu *hili*, na unajaribu hili, na kuelekea *huku*, na kukimbia hapa, na kukimbia pale. Bado hauna imani! Bali wakati . . . hiyo ndiyo tunayoita “Imani.”

³⁸ Mi-mi-mi . . . (kunradhi). Nawatakeni . . . (asante, ndugu).

³⁹ Mi—mimi nawatakeni mpate hili sasa. Sisi . . . kanisa halina budi kujiinua lenyewe katika uweza wa Mungu. Vipi? Tumekaribia sana mwisho, sasa; na nafikiri Kanisa limefikia mahali ambapo tunaweza kulifundisha mambo yenye kilindi kidogo, na kupangusia mbali baadhi ya huku kutokuamini

(mnaona?) na kufikia jambo fulani halisi. Unaona? Haina budi kuwa jambo unalolijua!

Na kama ukisema, “Ndugu Branham, hiyo si nuru.”

“Hata hivyo ninajua ni nuru.”

“Wajuaje ya kwamba ni nuru?”

“Ninaitazama.”

“Vema, wajuaje ya kwamba haungalikosea?”

“Macho yangu daima yameniambia mimi ya kwamba hiyo ilikuwa nuru.” Unaona?

⁴⁰ Na hiyo ndiyo sababu naamini hayo maono, maana kila mara yametangazwa kuwa kweli, maana yanatoka kwa Neno. Na kama Yeye analisema, hiyo yatosha. Basi, inapotangazwa hivyo, hamna tena kubahatisha, itakuwa hivyo. Kisha unasikia “BWANA ASEMA HIVI,” waona, kwa sababu ina—inapita mawazo ya binadamu. Imefikia milki ya mawazo ya Bwana. Bali unasimama hapa, kama tu Mzabibu...kama tu tawi likizaa tunda lililo katika mzabibu. Waona? Mungu humtumia mwanadamu, na mwanadamu pekee. Mungu hatumii mitambo. Mungu hatumii makundi ya watu. Mungu hatumii madhehebu. Mungu hutumia watu binafsi, kila mara!

⁴¹ Sasa, imani ni kuwa na hakika ya mambo, na kwa hiyo, twafahamu, mambo hayo yote yanafanywa. Si ma—mawazo, ni jambo lenyewe; hasa Imani Kamilifu. Hayo ndiyo ninayonena usiku wa leo, *kufikia Imani Kamilifu*. Si mawazo.

⁴² Sasa, wengine, watu husema, “Lo, nina imani; lo, bila shaka ninayo.” Vema, mbona unasimama hapa, basi? Unaona? Onaona? Onaona, matendo ya—yako yanathibitisha ya kwamba huna yale unayonena habari zake. Waona? Kama ulikuwa na imani, basi ya nini kusimama kwenye mstari wa maombi? Waona? Ya nini kufanya mambo haya?

⁴³ Unaona, kama ungalikuwa na Imani Kamilifu, ungalimtaazama Mungu moja kwa moja na kuamini, na kuenda zako. Haunge—haungehitaji kuja kwenye mstari wa maombi. Haungalihitaji mambo haya yote, kwa maana imani yako imeyafanya kuwa hivyo. Waona? Ingenifaidi nini kusema, “Inanipasa kuvaa shati?” Nimevaa shati!

⁴⁴ “Unajuaje una shati?”

⁴⁵ “Vema, ninaiona, naisikia, nami najua iko pale.” Vema, huwa dhahiri hivyo wakati Imani Kamilifu inaposhika hatamu. Hau—hauhitaji tena. Imetendeka tayari, unajua hivyo.

⁴⁶ “Unajuaje?”

⁴⁷ “Imani huniambia hivyo!” Ndiyo hiyo. Mnaona? Mnafahamu, ninayomaanisha? Hiyo Imani Kamilifu.

⁴⁸ Sasa, kwa maneno mengine, mimi najasiria, “Vema, nitakwenda. Biblia ilisema, ‘Waite wazee, na wampake mafuta,

wamwombee.’ Najua, nitaenda kule.” Nawe useme, “Vema, nitapona.” Unaona, unajifanya mwenyewe; usipoangalia sasa, u—utajichochea tu. Kisha utakapopitia hapa, useme, “Lo, bado sisikii...?...” Unaona, basi, ndiwe huyo, haukua na imani!

⁴⁹ Imani yako halisi italitenda papo hapo. I—imani yako halisi itaifanya dhahiri sana hata...Mtazame yule maskini mwanamke mwenye kutokwa na damu, alisema, “Nikigusa tu upindo wa vazi Lake, nitapona.” Na mara alipofanya hivyo, alisema “alijisikia mwilini mwake ya kwamba kutokwa na damu kumekoma.” Yeye hakika aliamini hilo.

⁵⁰ Naye alipougusa...kuthibitisha ya kwamba kulikoma—kukakoma, Yesu aligeuka akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Hiyo Imani Kamilifu! Na Imani hiyo hiyo Kamilifu usiku wa leo, itamgusa Yesu Kristo kama tu ilivyofanya wakati huo. Huyo mwanamke alikuja na Imani Kamilifu kwa wakati huo.

⁵¹ Sasa, sasa tunaona, hapo kwanza wanafunzi hawakuwa na hii Imani Kamilifu. Hawakuwa nayo, kwa maana walikuwa na Kristo, wakitembea pamoja Naye; Bali baadaye, Kristo alikuwa ndani yao. Na kwa hivyo, unaona, ni vigumu basi kuwa na hii Imani Kamilifu bila Roho Mtakatifu; hana budi kuileta, huileta. Sasa, unasema, “Je, wanafunzi hawakuwa na Imani Kamilifu?” La; kwa maana walikuwa na mtoto mwenye kifafa pale, ambapo walikuwa wakijaribu kumtoa huyu pepo kwake, na hawakuweza.

⁵² Naye babaye akamwona Yesu akija, akasema, “Tumemleta mwanangu kwa—kwa wanafunzi Wako, nao hawakuweza kumponya.” Mnaona?

⁵³ Na baadaye, wanafunzi wakamuuliza Yesu, wakisema, “Mbona hatukuweza kumponya?”

⁵⁴ Naye Yesu akasema, “Kwa maana, ya kutokuwa na imani, kwa kutokuamini kwenu.” Hiyo ni kweli. “Kwa kutokuamini kwenu kwa...”

⁵⁵ Sasa kumbukeni, wao walikuwa na nguvu. Yesu alikuwa amewapa nguvu kuponya wagojwa, kufufua wafu, na kutoa pepo, siku chache tu hapo awali. Wao walikuwa na nguvu, bali si imani ya kutumia hizo nguvu. Naam, ndivyo yalivyo Maskani ya Branham! Ndivyo lilivyo Kanisa, Bibi-arusi, leo! Roho Mtakatifu yuko hapa na hizo nguvu, bali hamna imani ya kuzifanya zitende kazi. Mnaona ninayomaanisha? Inachukua imani kuzifanya zitende kazi.

⁵⁶ Hapa: nina risasi nilizozishindilia. Ninajua vile zitakavyofanya kwa sayansi yake, kama Neno, bali sina budi kuifyatua bunduki. Moto hauna budi kuingia kwenye baruti. Baruti ina nguvu, bali haina budi kupata moto kuiwasha. Na jambo lile lile, hiyo baruti imo katika risasi, bali itahitaji imani kuitia moto na kuitupa nje. Hiyo ndiyo inayohitajika (mwaona?).

Imani Kamilifu kuwasha baruti ya Roho Mtakatifu ambaye tunaye sasa, kwa kuwa ametujilia sisi; imani ya kuiwasha, kuona mambo makuu, ni ku... imani, kitu ambacho kinaikabidhi kwako.

⁵⁷ Ukiwa mwenye moyo uliojaa furaha, unaingia kwenye chumba cha wagonjwa, ukijua hasa utakayosema. Unaingia mle ukijua kitakachotendeka, jambo fulani limekwisha kufunuliwa, nawe walijua. Nawe unaingia, “Katika Jina la Yesu Kristo, inuka kutoka hapo. BWANA ASEMA HIVI!” Ndiwe huyo; hiyo ni Imani Kamilifu. Kama kungalikuwa na watu milioni kumi wamesimama pale wakisema haitatendeka, wewe unajua itatendeka kwa vyo vyote maana unajua hivyo. Itatendeka. Haijalishi yale mtu ye yote anayosema, ni wewe uliye na hiyo imani.

⁵⁸ Ungaliwazia, Yoshua, angewaita wazee wa Israeli na kusema, “A-haa, ndugu zanguni, sisi ni watumishi wa Bwana, ningewatakeni msemi...mumuulize Bwana kama ingekuwa vema iwapo alitupa nuru nyingine zaidi, mwaona, na kusimamisha jua kidogo?”

⁵⁹ Hasha; yeye aliliihitaji (na bila maombi, bila cho chote), aliliihitaji, naye akaamuru tu jua! Akasema, “Simama pale! Nina haja, nami nimo katika utumishi wa Bwana, Naye alinituma humu kufanya hii kazi, nami ninafanya vizuri niyuavyo, na adui amekusanyika tena, nao wako hapa; nikiliacha jua litue, wao wataungana na kunipa shida zaidi. Hivyo basi, simama kimya!! Na, mwezi, wewe simama kule!” Amina; na ukatulia kwa masaa ishirini na manne.

⁶⁰ Naam, kama ulimwengu unazunguka-zunguka naye aushikilie, nalo jua likae mahali pamoja na lisizunguke, ilikuwaje basi? Sasa ulijifanya mwenyewe kafiri, kama ukisema hivi; halafu kama hufanyi hivyo, basi unajipumbaza kwa sayansi, kwa maana wao walisema ulimwengu ukisimama, utaanguka. Nini basi? Na ukisema Neno la Mungu si kweli, basi wewe ni kafiri. Waona? Bali ilitendeka, hilo ndilo jambo muhimu. Sijui ilivyotendeka, bali ilitendeka!

⁶¹ Sijui Roho Mtakatifu afanyavyo kazi, bali najua alishuka juu yangu. Si—sijui ilivyotendeka, bali najua baraka Zake. Hayo—hayo tu ndiyo ninayotaka kujua, ni baraka za Roho Mtakatifu. Na anavyotenda, jinsi Yeye anavyotenda kazi, hiyo ni siri Yake.

⁶² Huyu kijana hangaliponywa, kwa maana... Hao wanafunzi walikuwa na nguvu; Yesu alikuwa amewapa nguvu kuponya namna zote za magonjwa, kutoa pepo, kutakasa wenye ukoma, na kufufua wafu. Yeye aliwapa nguvu, bali hawakuwa na imani kuendeleza nguvu walizokuwa nazo. Kisha wao wakamswali Yesu na kusema, “Vema, basi, mbona hatukuweza?”

⁶³ Sasa kumbukeni, wao walikuwa na Neno; nalo Neno lilikuwa Mwili wakati huo. Nalo Neno likawaambia, “Nawapa *ninyi*

nguvu.” Amina! “Nawapa *ninyi* nguvu.” Na walikuwa na nguvu bali hawakuwa na imani ya kuliendeleza Neno lililokuwa ndani yao. Mnaona ninayomaanisha? Bali Yesu alikuwa nayo, Yeye alikuwa Neno, Naye alikuwa na imani ya kwamba aliyosema yatatendeka. Yeye alisema, “Lo, mlete hapa. Je, nitawavumilieni hata lini?”

⁶⁴ Yeye alikuwa na imani, pamoja na nguvu Zake. Alifanyaje? Alisema, “Siwezi kutenda neno Mwenyewe.” Kwa nini? Yeye alitegemea kile alichokuwa; alitegemea ujuzi kwamba Yeye alikuwa Neno. Naye alikuwa na imani katika Mungu, aliyemfanya Yeye Neno. Yeye alikuwa Mungu (Neno), nayo ilikuwa ndani Yake, na hiyo ilimpa Yeye imani kwa maana alifahamu mahali Pake. Yeye alijua kile alichokuwa, kwa maana Maandiko yalikuwa yamesema Yeye alikuwa hivi. Na hapa kila Andiko liliungana, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa hasa yale Maandiko yalisema angekuwa, Naye alijua kile alichokuwa.

⁶⁵ Kwa hivyo, Yeye alitegemea yale Mungu alimfanya. Na ikiwa Yeye alifanya hivyo, basi, hatuwezi kutegemea kile Mungu ametufanya alifanya kama waaminio? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio!” Yeye alikuwa na imani kwa yale aliyokuwa. Na iwapo u mwamini, una imani na yale uliyo: wewe ni muumini! Naikiwa una imani katika Mungu, Biblia inasema hapa katika... “Ikiwa—ikiwa mioyo yetu inatuhukumu, basi hatuwezi kuwa na imani; bali kama mioyo yetu haituhukumu, basi tuna imani; tuna ujasiri kwa Mungu.” Kama unataka kusoma hayo, yanapatikana katika Mt. Yohana 3:21. Nimeandika hilo Andiko hapo chini.

⁶⁶ Sasa tazama, Yohana Mt...namaanisha 1 Yohana 3:21. Tazama:

...Mioyo yetu isipotuhukumu, tuna ujasiri kwa Mungu.

⁶⁷ Bali mradi tu unafanya mambo mabaya, hauwezi kuwa na ujasiri kwa Mungu. Kwa hivyo, unaona, unaweza...bila shaka utajua ya kwamba umekosea. Unajiweka nyuma kule kama mwenye dhambi, kwa kujua ya kwamba umekosea. Bali moyo wako usipokuhukumu, nawe unajua ya kwamba u muumani, na hamna neno kati yako na Mungu, unaweza kuomba utakacho na utapewa, kwa sababu ni Neno ulilopewa kama tu lilivyopewa wale wanafunzi.

⁶⁸ Sasa, jambo pekee unalopaswa kufanya basi, ni kuwa na imani na kile ulicho. Uwe na imani katika kile Neno linasema ulicho! Naye Yesu alikuwa na imani katika Neno la Mungu, lililosema alichokuwa, “Nimeandikiwa.” Je, Daudi, katika Zaburi; na manabii na wengine wote hawakiunena habari zake? “Mimi Ndimi Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni.” Amina! “Mimi Ndimi ule Mti wa Uzima katika Shamba la Edeni. Mimi ni mambo haya yote,

“MIMI NIKO AMBAYE NIKO.” Naye alijua kwa hiyo Imani Kamilifu, ya kwamba Yeye alikuwa Masihi aliyetiwa mafuta, ambaye Roho wa Mungu alikuwa juu Yake. Yeye alisema, “Sasa, Mimi, Mwenyewe, siwezi kufanya kitu; bali ni imani Yangu katika Mungu.” Naye Mungu alikuwa ndani Yake, Neno lililodhihirishwa. Na Neno la Mungu linapokuja ndani yako, linadhihirishwa, kwa maana wewe ni muumini. Waona? Na *muumini* ni “imani ya Mungu inayotenda ndani yako.”

⁶⁹ Mnapenda hilo? Na—na—napenda wakati ninyi . . . napenda kufundisha ambapo . . . jinsi . . . imani ni nini hasa.

⁷⁰ Alijua Yeye alikuwa nani, bila shaka kamwe, Yeye alijua alikuwa Mwana wa Mungu. Alijua hivyo, kwa maana Neno lilimtambulisha. Neno la Mungu lilimtambulisha Yeye alikuwa nani. Yeye alisema, “Kama sikitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini; bali—bali nisipozitenda hizo kazi, msiniamini. Bali nikizitenda, basi ziaminini zile kazi, kwa maana ndizo Neno lililoahidiwa likidhihirishwa.” Lo, laiti mngaliamshwa na hilo! Dakika moja. Mnaona, Neno lenyewe lilimtambulisha, kwamba alikuwa Nani. Naye alisema, “Ni nani awezaye kunihukumu kwa ajili ya dhambi?” Kwa maneno mengine, “Ni nani awezaye kunionyesha ya kwamba maisha Yangu na kazi Zangu hazitimizi yale Masihi anayopaswa kutenda?” Hamna mtu angaliweza kusema cho chote; kwa maana alikuwa hivyo. Ndipo alikuwa na imani kuamini, basi; na cho chote alichosema, kilitendeka.

⁷¹ Kisha akageuka na kusema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Kitambo kidogo, na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mtaniona, kwa sababu nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Msifikiri mtakavyosema, si kazi yenu kunena, ni Baba yenu anayekaa ndani yenu, ndiye anenaye. Na si Mimi, ni Baba akaaye ndani Yangu, ndiye atendaye kazi.” Mnaona mnaona ninayomaanisha?

⁷² Basi, utambulisho wa Mkristo wa Kimaandiko, Maneno haya alisema Yesu: “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Naam, unawezaje kujiita mwamini, watu, na kukana Maneno hayo? Unawezaje kujiita mwamini na kukana lo lote la Neno hili? Unaona? Hauwezi kufanya hivyo. Wewe si mwamini, kwa hivyo ishara haziwezi kufuatana nawe, kwa maana wewe hukubali tu yale unayotaka kuamini na kuacha mengineyo . . . hauta—huamini. Bali inakupasa kuchukua jambo lote, na kuliadini. Na unapoamini kweli kweli (si kujifanya mwamini, bali kuamini kweli kweli), basi ishara hizi hufuatana na hao waaminio.

⁷³ Lo, ungaliweza kulinganisha Mkristo leo na hao Wakristo wa zamani za kale? Jinsi hao mitume walivyotembea katika uweza wa Roho, wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Mfungwa tu, kama nilivyohubiri usiku uliopita, mfungwa kwa Neno na mapenzi ya Mungu; yeye hangaliondoka hadi Mungu amwondoshe. Je, haungalitaka kuona Kanisa likiinuka hivyo? Litainuka; litarudi.

Ha—halina budi kutokea. Hiyo ni kweli. Halina budi... Liko njiani sasa. Naamini.

⁷⁴ Kwa maana Neno lilimtabulisha, lilimtambulisha, alivyokuwa; na Neno lile lile hututambulisha sisi. Mnaona? “Mtu akinipenda, atazishika amri Zangu. Na kama akisema ananipenda, na hazitii amri Zangu (Hiyo ni zote), yeye ni mdanganyifu, na Kweli hata haimo ndani yake.”

⁷⁵ Ukisema, “Vema, siamini yote...” Vema basi, hiyo... wewe ni asiyeamini, hiyo tu. Kama Biblia ilisema hivyo, hiyo inaifanya kweli, hiyo yatosha Milele. Yale Biblia isemayo, ni Kweli.

⁷⁶ Tazama ambapo Yeye alituambia, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu.” Yohana 15, “Kama mkikaa ndani Yangu,...” (Mnaona, mwaminini Yeye). “Kaeni ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, kisha *ninyi* ombeni lo lote mtakalo.”

⁷⁷ Sasa, mnaona, Yeye alijua alikuwa nani, kwa hivyo Yeye alikuwa na imani. Imani ingalizaa mazao alipojua Yeye alikuwa nini. Basi, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani Yenu,” ndipo mtajua ninyi ni nani. Ombeni mtakalo, mtapewa.

⁷⁸ Si hiyo ingekuwa ajabu, usiku wa leo, kama kila mtu angalipitia kwenye huo mstari wa maombi, aseme, “Mimi ni Mkristo. Sina hukumu ya dhambi. Najua—najua moyo wangu haunihukumu. Kitu fulani kinaniambia ya kwamba leo ndio mwisho wa mateso yangu?” Hiyo ni... ukiamini, utaondoka hapa ukiwa na kitu fulani. Haidhuru jinsi utakavyokuja kwa mwamsho, jinsi utakavyofanya, haitafaa kitu hata hiyo Imani Kamilifu imejidhihirisha na kujitambulisha yenyewe ndani yako, kama jambo dhahiri. Na itakapofanya hivyo, hamna kitakachokutisika kutoka kwake.

⁷⁹ Kama—kama ulikuwa na kansa, na daktari akakwambia jana ya kwamba ugekufa kabla Jumatatu asubuhi, (moyo wako wote, kupumua kumekwisha, umeliwa na kansa, damu yako imejaa kansa kabisa, cho chote kile); na Kitu fulani kije na hakika hii ya imani halisi, ile Imani Kamilifu ilifanywa kitu dhahiri ndani yako, ungalicheka mbele ya huyo daktari.

⁸⁰ Ungekuwa kama Eliya wa kale, alipokwenda juu chini mbele ya ile sanamu, akasema, “Mbona msiitane kwa sauti kuu zaidi kidogo? Na huenda ikawa ana shughuli.” Yeye alijua yale angalifanya, kwa maana Mungu aliisha kumwambia yatakayotendeka. Yeye akasema, “Na mungu yule ajibuye kwa moto, awe Mungu.”

⁸¹ Wao wasema, “Tutashika shauri hilo.” Nao wakamwaga maji juu ya madhabahu. Kisha wa—wakajikata-kata, nao wakafanya kila kitu, na kuita, “Ee Baali! Ee Baali! Jibu!!”

⁸² Eliya alikuwa ametulia tu kama alivyoweza kuwa. Yeye akasema, “Mwiteni kwa sauti kuu zaidi,” ka—kasema, “huenda

ikawa ana shughuli. Hu—huenda ikawa ameenda kuvua samaki. Labda anafanya jambo jingine, mwaona. Ameenda zake mahali fulani.” Wao... Akawafanyia tu dhihaka, kwa sababu alijua itatendeka.

⁸³ Lo, tazama wakati alipotayarisha kila kitu. Aliondoka akaenda pale na kusema, “Bwana Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Israeli!” Yeye hakumtaja kwa jina lake *Yakobo*, “mdanganyifu.” Alimwita *Israeli*, “mtawala kwa Mungu.”

⁸⁴ “Bwana Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa huyo Mtawala (Yakobo), na ijulikane leo kuwa mimi ni mtumishi Wako; nami nimefanya haya, si kwa mapenzi yangu, si kuyabuni, bali kwa neno Lako nimefanya hili; mapenzi Yako, uliniambia la kufanya. Ulinionyesha mambo haya yatukuwa hapa. Sasa, nimemwaga maji juu ya madhabahu. Nimefanya mambo haya yote kwa amri Yako. Sasa, na ijulikane!” Na aliposema hivyo, moto ukashuka kutoka Mbinguni. Yeye alikuwa na matumaini kabisa ya kwamba ungeshuka, kwa sababu alikuwa na hakika ya mambo. Kwa nini? Neno lilisema hivyo.

⁸⁵ Basi, Biblia ii hii ni Neno lile lile la Mungu. Na unapoweza kupokea hakika ya mambo (hiyo ni Imani Kamilifu); hakika ya mambo kwamba ahadi hii ambayo Mungu aliifanya ni *yako*.

⁸⁶ “Unajisikiaje, Ndugu Branham, unaposimama pale na kuona watu wakija wa lugha mbali mbali na kadhalika? Je, unaogopa?” La, bwana. La, bwana. Yeye alisema hivyo! Sijaogopa bado, maana Yeye aliniambia hivyo, nami naamini ya kwamba ni Kweli.

⁸⁷ Kama Yeye angaliniambia usiku wa leo, kwenda kwenye kaburi la rais na kumfufua George Washington kesho asubuhi, ningalivalika ulimwengu mzima, “Njoooni muone ikitendeka.” Ningalisema, “Leteni kila mpinzani... leteni—leteni kila mpinzani muwezaye mkawasimamishe hapa karibu, mtaona Utukufu wa Mungu. Wekeni kile kiti hapa upate kuketi na kupumzika muda kidogo; yeye atakuja hivi punde, mara nimwitapo.”

⁸⁸ Usiku huo wakati yule mvulana mdogo kule Finland, siku hiyo, hasa; amelala pale maiti, alikuwa amelala pale nusu saa, amepondwa-pondwa, damu ikimtoka machoni, puani na maskioni; miguu yake midogo imevunjika, ndani ya maskini soksi zake ndefu; na nyayo zake zikitokeza mwishoni mwa soksi zake, hana viatu. Nalitazama, nami nikawazia, “Yule hana budi kuwa ndiye yule mvulana.” Nikasema, “Aisee, hebu tutazame nyuma ya Biblia hiyo, Ndugu Moore.”

⁸⁹ Tukamwita Ndugu Lindsay, Ndugu Moore akatazama nyuma kule: “‘Na itakuwa kwamba,’ BWANA ASEMA,” (Lo, jamani!) “Kutakuwa na n—nchi ambamo mna miti mingi yenye majani mabichi. Miamba imelundikana. Mvulana mdogo aliyenyolewa vyema sana, kijisuruali kidogo kilichofungiwa

hapa kuinoni, na miguu yake...soksi zake zimevutwa juu. Atakuwa na macho ya hudhurungi, yatakuwa yamegeuzwa. Atauawa katika ajali ya motokaa. Bali kamwekee mikono, naye atafufuka.”

⁹⁰ Ndilo Hilo, limeandikwa mle. Alilala pale, amina, akingoja tu Neno. Nikasema, “Kama huyu mvulana hataishi katika muda wa dakika chache tangu sasa, basi mimi ni nabii wa uongo, nifukuzeni Finland. Bali akiishi, pigeni magoti mkatubu!”

⁹¹ Nikasema, “Mauti, hauwezi kumzuia.” Nikaiita roho yake kulingana na Neno la Mungu, “Katika Jina la Yesu Kristo,” na akaruka juu. Sawa! Mwaona, . . . ? . . . Imani, mwaona, ikashika hatamu. Mungu alisema hivyo, ndiyo hiyo!

⁹² Naam huyo—huyo ni Mungu akinena siku hizi katika ono. Lakini hili: kama hilo ono halikupatana na *Hili*, hilo lingekuwa kosa; *Hili* ni zaidi ya ono. Kama ono lo lote haliambatani na Neno, uliachilie; halikutoka kwa Mungu, Mungu hapingi Neno Lake Mwenyewe. Kwa hivyo, kama Neno hili lilikwambia jambo fulani, basi waweza kuwa na matumaini yale yale basi kile kitakachotendeka. Hamna kitu . . . kama linasema, “Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya”; vema, ndugu, kama imani, hiyo Imani Kamilifu, ingalishika hilo, unge. . . upitiapo kwenye mstari huu wa maombi, ungalikuwa unaruka-ruka na kupasa sauti hata ulipoondoka hapa, “Imekwisha!” Imekwisha, yote imekwisha! Imemalizika! Kama ulikuwa na haja moyoni mwako na unaamini ya kwamba hayo maombi yalipofanywa, yangejibiwa, hamna jambo lo lote unalozungumza, hilo ndilo litakalotendeka; kama mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu.

⁹³ Yesu alikuwa na Imani Kamilifu. Ye—Yeye alikuwa nayo, nayo ilikuja kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Nawe unakuwa Neno; unakuwa Neno, unapopokea Neno. “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu. Maneno Yangu ambayo. . .” (*hili* Neno) likikaa ndani yenu, basi ombeni mtakalo, nanyi mtapewa.” Mwaona? “Mkiuambia mlima huu, ‘Ondoka,’ na msiwe na shaka, bali muamini katika yale mmesema, basi mtapokea mlichosema. Muombapo, aminini mta pokea mlichouliza, mtakuwa nacho, mtapewa.” Wakati, mahali, hamna kitu kitakachokibadilisha. Unajua kimetendeka. Tayari—imekwisha tayari.

⁹⁴ Sasa, tazama! Sasa, Naye akatwambia, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu;” (Yohana Mt. hapa) “Unaweza kuomba utakacho, kitatendwa.” Basi, tambua mahali pako katika Maandiko, kama mwamini. Unaona, huna budi kutambua mahali pako, kama Yeye alivyotambua mahali Pake.

⁹⁵ “Si imeandikwa ya kwamba Kristo atakuja, na yote Kristo atakayofanya?” Alimwambia Kleopa na wengineo asubuhi hiyo, “Je! haijaandikwa katika Maandiko ya kwamba itawapasa

hao...ya kwamba imempasa kupata mateso kisha auawe na kufufuka siku ya tatu?" Kasema, "Mbona mmekuwa msiofahamu?"

⁹⁶ Nao wakawaza, "Jamani, mtu huyu anazungumza tofauti kidogo na watu wengine." Wakang'amua, walipoingia mkahawani, alikuwa Ndiye. Mnaona, macho yao yalifumbwa wasimtambue. Mwaona, wao walijua Yeye aliendelea kunukuu hayo Maandiko, nao wakajua Ndiye.

⁹⁷ Basi, huna budi kuamini ulichoomba. Iwapo wewe ni mwamini, jitambue mwenyewe kama mwamini. Tambua ya kwamba mambo haya ni kwa ajili yako. Iwapo kuna hukumu ya dhambi maishani mwako, yanyoshe hayo kwanza. Waona? Iwapo moyo wako unakuhukumu... mimi... ama waweza kuwa na Oral Roberts na—na watu wengine dazan walio na imani kuja hapa na kukuombea, na kuruka juu chini, na kukumwagia galani za mafuta, bali ha—haitafaa kitu. Hiyo ni kweli.

⁹⁸ Nini kinachotokea cha hayo kwenye mikutano ya Oral? Nakipata kwenye mstari wa maombi. Unamsikia akisema ya kwamba alikuwa amekwisha kuombewa hapo awali.

⁹⁹ "Mtu mwenye nywele nyeusi, mtu mkubwa, mwenye taya kubwa." Huyu ni Oral Roberts. Mwaona? "Na hiyo ilikuwa katika mji *fulani*; unaitwa kitu *fulani*."

¹⁰⁰ "Naam, hiyo ni kweli." Mwaona?

¹⁰¹ "Uliombewa na mtu *fulani*." Mnaona, hivyo. "Bali shi—shida yako ndiyo hii." Waona? "Nenda katengeneze jambo hilo. Nenda kule ukatubu hiyo dhambi kwa mumeo, kwa mkeo. Nenda kafanye jambo hili." Haitakufaa cho chote, haidhuru ni nani anayekuombea, hata utakapotengeneza hilo. Hukumu iko moyoni mwako, na Mungu hataingia katika moyo huo unaohukumika. Waona? Mungu hakai katika huo; huna budi kuutengeneza. Basi utakaposuluhisha hilo, ni lazima uwe na imani. Kama kila kitu ni sawa, huna budi kuwa na imani na kuamini. Usiogope.

¹⁰² Katika Kitabu cha Ayubu, inasema hapa, "Ayubu aliogopa." Na kile alichogopa, kilitendeka kweli. Nini kilisababisha hayo? Uoga wake. Huo ndio ulisababisha. Imani yake ingalimlinda kutoka kwa hayo, bali uoga wake ukamleta... ukamletea hayo. Aliogopa itatukia, na ikatukia. Sasa, kama ilikuwa—alijua haingetendeka, haingetendeka. Mwaona ninachomaanisha?

¹⁰³ Iwapo una uoga unapokuja kwenye mstari wa maombi, "Labda hata sina imani ya kutosha;" haitatendeka kamwe, usijisumbue. Unaona? Bali kama unajua itatendeka, itatendeka. Waona? Waona, ni kuwa na hakika ya jambo *fulani*. Ayubu aliogopa kwamba mambo haya yangemtokea, nayo yakatokea. Kama unaogopa kwamba ugonjwa wako utakuacha... ama hautakuacha, hautakuacha. Iwapo una imani, kwamba utakuacha.

104 Muulize daktari ye yote wa madawa. Jambo la kwanza atakalokufanya ufanye kwanza, ni kuwa na matumaini kwa madawa atakayokupa. Iwapo huna matumaini nayo, afadhali uyaache. Waona? Bila shaka! Ni nini basi? Ni imani inayoponya; ni imani inayofanya hivyo wakati wote.

105 Petro, alikuwa akiendelea vyema hata alipoanza kuogopa. Neno lilimwambia, angetembea majini. Hapo kwanza aliogopa, alidhani ilikuwa pe—pepo, naye akasema, “Bwana, ikiwa ni Wewe, niamuru nije Kwako juu ya maji.”

106 Kasema, “Njoo.” Naam, hiyo ni kama tu Yakobo 5:14, ni kama Marko 16; ni Mungu yule yule aliyesema hayo, kasema, “Njoo.” Kwa hivyo basi akaanza kwenda kwa miguu. Alifanya vema, akashuka chomboni, akaanza kwenda kwa miguu. . .

107 Kulikuweco dhoruba baharini, mwajua; mawimbi meupe makubwa sana, makubwa kuliko vilima hivi vilivyo humu, povu zikivunja juu yake; za kutisha, huenda ikawa povu zenye urefu wa futi kumi na tano ama ishirini, povu zikivunja. Na hilo lilikuwa jambo la kuogofya kwake kusema, “Ikiwa ni Wewe, Bwana. . .” Unaona, Yeye alionekana kama. . . ilionekana kama kivuli ama pepo. Yeye akasema, “Ikiwa ni Wewe, niamuru nije Kwako juu ya maji.”

108 Yesu akasema, “Njoo.”

109 Naye akashuka, kasema, “Ni Bwana, nitatembea tu.” Bali alipoelekeza macho yake kwenye mawimbi, akaogopa. Aliwaza nini niani mwake? Jambo la kwanza, yeye. . . “Nitatembea kwa sababu Neno lilisema nitembee.” Na jambo la pili, alitazama haya. . . vema, alitazama dalili zake; alitazama kule na kuona jinsi mawimbi yalivyokuwa, naye akaogopa; na alipofanya hivyo, akazama. Waona? Alichooogopa, kikatendeka! Alichoa mini, kikatendeka! Alipoa mini ya kwamba angetembea, alitembea; alipoa mini. Akahofu katika imani yake, kisha uhakika wake wa mambo ukamwacha. Unaona? Alikuwa angali anakiri imani yake, bali hakuwa na hakika ya mambo. Hiyo hakika ya mambo ingaliruka juu ya yale mawimbi makubwa meupe na kumwendea Yeye, waona, iwapo ana Imani Kamilifu. Unaona? Bali hakuwa nayo. Alifikiri anayo. Alifikiri hivyo kwanza, alikuwa tayari kudiriki kwenda, “Naam, *Bwana* aliniambia nifanye hivyo, haina budi kutendeka.” Kwa hivyo akashuka chomboni moja kwa moja, akashika njia akaenda. Yeye hakuyajali ya—ya—ya—yale mawimbi, jinsi yalivyokuwa kinyume. Hakuwaza hayo kamwe niami mwake.

110 Basi, unapoanza kuwazia, “Vema, sasa ngoja. Na, wajua, nimekuwa mgonjwa kwa muda mrefu, mimi. . .” Koma! Hata ingelifaa kama ungalirudi chomboni. Unaona, waona? Bali unapocha kuwazia hilo, . . .

111 “Ibrahimu hakufikiria hali ya mwili wake, uliokwisha kufa, wala hali ya kufa ya tumbo lake Sara.” Yeye hakuwaza

hayo, hata hakuyafikiria. Hata hayakuletwa kwenye—ufahamu. Hata hakuyafikiria; yeye alifikiria tu yale Mungu aliyosema, naye akasonga mbele. Hiyo...mradi tu Petro alifanya hivyo, alitembea.

¹¹² Yesu aliishi katika ulimwengu usiojulikana na mtu ye yote, alikuwa mtu wa kipekee. Aliishi katika ulimwengu wa Imani Kamilifu katika Mungu Mkamilifu, aliyekuwa ndani Yake. Kama tungaliishi katika Imani Kamilifu ya Mkristo, tulivyo, tungalikuwa watu wa wasiofahamika ulimwenguni; watu hawangalikufahamu. Ungalitembea katika Roho. Yale aliyosema Roho, ungetenda. Aliyokataza, haungeyafanya. Watu wangeanza kusema...wao...ungekuwa m—mtu asiye fahamika kwao.

¹¹³ Hivyo ndivyo ilivyo kwa waamini wote, wao hawafahamiki. Watu hawafahamu, maana wanaishi katika ulimwengu wao wenyewe. Yesu aliishi katika ulimwengu ambao hamna mtu mwingine angaliweza kuugusa. Wanafunzi hawangalimfahamu. Aliponena pamoja nao, walisema *hivi*. Kisha wakasema, “Naam, Wewe hu—hunena kwa mafumbo! Ha—hatufahamu hili. Hili linawezekanaje?” Mnaona, wao hawakuwa katika ulimwengu alimoishi. Unaona, hawangalimfahamu, hamna mtu angalimfahamu.

¹¹⁴ Na kwa hivyo mtu anapoishi kwa imani na kuenenda kwa imani, namaanisha imani yenye uhakika wa mambo, yeye anatengwa na ulimwengu mzima na akawa kiumbe kipya katika Kristo. Hapo, sasa unafikia asili ya Bibi-arusi. Unaona? Unafikia katika hali ya kunyakuliwa, sasa. Hiyo inamaanisha kila mmoja wetu (si mchungaji tu, sasa), mashemasi, wadhmini, hiyo inamaanisha washirika, kila mtu binafsi anatembea katika ulimwengu fulani pamoja na Mungu peke yake. Unabatizwa katika Ufalme huu, na hamna mtu ndani isipokuwa wewe na Mungu. Waona? Yeye hutoa amri, nawe unazitekeleza. Cho chote asemacho, hamna tashwishi kamwe, unatembea moja kwa moja. Kama Bwana akisema *hivi*, hamna mtu ulimwenguni angaliweza kukushawishi vinginevyo, unaendelea tu vivyo hivyo. Sasa unafikia Imani Kamilifu, ukamilifu mtimilifu usioweza kushindwa. Imani *hiyo* haishindwi. Naam, Yeye alikuwa mtu asiye fahamika kwao na Imani Yake Kamilifu; basi ndivyo ilivyo kwa hao wenye Imani Kamilifu, wao ni watu wasiofahamika kwa wengine.

¹¹⁵ Tumefundishwa “mpingeni shetani, naye atatukimbia.” Naam, *kumpinga* ni “kumkataa” tu; *mpinge* tu, hiyo ni kusema, “toka kwake.” Mungu alisema jambo fulani; haidhuru anayotaribu kukwambia, hata usimsikize. Inakupasa...masikio yako ni bubu kwa kinginecho chote isiopokuwa neno analosema Roho. Unaona? “Kwake yeye aliye na sikio (linalosikiza), aone neno ambalo Roho ayaambia makanisa”; yeye aliye na mahali

pa kusikizia, ambapo panapokea neno ambalo Roho ayaambia makanisa. Waona?

116 Yale shetani asemayo, “Vema, siwezi hata...” Hilo halihusiani nalo... “Vema, ukifundisha hayo, dhehebu litakuweka wewe...” Hilo halihusiani nalo, yeye anasonga mbele tu.

117 “Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho anayaambia makanisa.” Mwajua, katika Biblia, inasema kila mara hayo. “Yeye aliye na imani. Kwake aliye na sikio, na asikie,” Mnaona? “Yeye aliye na akili, na azihesabu hesabu za mnyama huyo.” Mambo haya yote mbali mbali. “Yeye aliye nayo, na awaambie hao wengine, wapate kujua.”

118 Na hiyo ni kwa imani tunayonena habari zake sasa, imani ambayo hauna budi kuwa nayo, ile Imani Kamilifu; ile Imani isemayo “Ndio!” Hamna kiwezacho kusema “La”, Mungu asemapo, “Ndio.” Unaona? Anaposema “Ndio,” ni “Ndio!” Na hamna kitu kinachoweza kuiondoa kwako.

119 Akiwa na hiyo Imani Kamilifu, Yeye alikuwa wa ajabu sana. Naye Ibilisi hakukaa karibu Naye kwa muda mrefu. Tulipata hayo katika somo asubuhi ya leo. Alipokuja na yale madanganyo makuu ya—ya mawazo ya kielimu, alimletea Yesu ulaghai alipokuja, naye akaona kwamba aligonga waya ya kipimo cha elfu kumi cha nguvu za umeme: zikamrusha nyuma tena. Naam, bwana. Naye akasema, “Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu!”—akapata ganzi basi.

Alimjia tena mpole kidogo, aliposema, “Naam, Wewe ni mtu mashuhuri, unaweza kujiweka hapa na uwe mtu mkuu.”

120 Kasema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani.” Lo, jamani, alichokikabili! Kisha, “Usimjaribu Bwana Mungu wako.” Waona, Yeye alijithibitisha Mwenyewe kwa Shetani ya kwamba Yeye alikuwa Bwana Mungu. Kwa maana imeandikwa, Usimjaribu...”

121 Naam, ka—kama Shetani hakujua ya kwamba huyo alikuwa Bwana Mungu, angalisema “Ngoja kidogo, wewe si Mtu huyo.” Bali yeye alijua bora kuliko kubishania hayo na Yesu.

122 Yeye alijua msimamo Wake. Akasema, “Usimjaribu Mungu Bwana wako.” Na hivyo ndivyo alivyokuwa. Na shetani alijua kuliko kusema hivyo, kwa maana kazi za Yesu tayari zilikuwa zimethibitisha ya kwamba Yeye alikuwa Bwana Mungu wako.

123 Tazama! Sasa nyingine, Imani Kamilifu ni mtawala wa kila hali. Imani Kamilifu hutawala hali zote. Haidhuru ni nini, huitawala. Sasa, tazama tu! Unapoamini cho chote, kufanya cho chote, na una imani katika yale ufanyayo; haidhuru hali ya mambo iko vipi, hilo halihusiani nalo kamwe. Waona, hutawala hali hiyo. Kama ni—ni katika chumba cha wagonjwa, na Bwana

akafunua ya kwamba hili jambo fulani litatendeka, linene tu na uendelele.

¹²⁴ “Lo je . . . ?” Usiulize maswali yo yote. Imekwisha, endelea tu kusonga mbele. Waona? Inatawala hali zote za mambo. “Vema, kama ukifanya *hili, fulani* atafanya . . .” Hiyo . . . mnaona, tayari imelitawala hilo. Waona?

¹²⁵ Imani huamini ya kwamba Mungu atalishughulikia. “Sijui jinsi atakavyofanya hivyo, bali atafanya hivyo kwa vyo vyote.” Mnaona? Inatawala hali zote za mambo.

¹²⁶ Na Imani na Upendo ni jamaa, kwa maana hauwezi kuwa na Imani isipokuwa uwe na Upendo, kwa maana Imani yako iko kwa Mungu Ambaye ndiye asili halisi ya Upendo. Imani na Upendo hutenda kazi pamoja.

¹²⁷ Bila shaka, kama tu mume na mke vijana. Mchukue kijana mwanamume na kijana msichana, nao wanapenda . . . wanapendana. Na wanapoendelea na kuanza kujuana wao kwa wao zaidi, mioyo yao inaanza tu kupiga-piga kama mmoja. Unaona? Wana—wana . . . bali bado si mume na mke, ila mapenzi yao yanawashikamanisha pamoja, nao wanaaminiana. Naam, iwapo wanapendana, kupendana kweli kweli, nawe wajua ya kwamba msichana huyu anakupenda na—naye anajua ya kwamba wewe wampenda, mna matumaini (mnaaminiana) mnaaminiana ninyi kwa ninyi; kama sivyo, afadhali msioane. Ona?

¹²⁸ Tazama, huna budi kuwa na imani. Nawe ukiwatenganisha na kumweka mmoja kusini kabisa na mwingine kaskazini kabisa, kungali na mapigo hayo ya upendo moja kwa mwingine, haidhuru wako wapi. Wao wangali waaminifu moja kwa mwingine kama wawezavyo kwa maana wanapendana. Na iwapo unampenda Bwana, si kujaribu tu kupa kuzimu, bali unampenda Bwana, basi una imani katika Mungu; waona, iwapo unampenda.

¹²⁹ Kama m—msichama kijana . . . ilitendeka tu hapa Louisville si muda mrefu uliopita. Mwanamke, yeye alikuwa—alikuwa . . . Mkristo kwa miaka mingi bali bwana wake alikuwa tu . . . wakapendana, akampenda mtu huyu. Aliisha kuwa Mkristo, miaka kadhaa. Na kwa hivyo wakaoana; walipendana na kuaminiana nao wakaoana. Na kwa hivyo huyo mwanamke akamwambia huyu mwanamume, kasema, “Mpenzi, lazima iwe ni vigumu kwako, wewe ni Mkristo mchanga. Unapitia katika majaribu mengi sana.” (Jambo ni kwamba, alikuwa akinywa pombe) Kasema, “Umekuwa na shida nyingi.” Naye kasema, “Ninajua inakupasa ujaribiwe vibaya sana.” Na akasema, “Nataka ujue jambo moja sasa. Basi, kama ukianguka, kama u—ukianguka katika majaribu na ushindwe, usikose kuja nyumbani; rudi tu. Njoo huku, kwa maana ni—nitakuwa mumu humu nikikungoja, nami nitakusaidia kuomba kabisa tena, hata

upate ushindi. Nitakaa pamoja nawe, kwa maana nilipokuoa, nalikuoa kwa sababu nilikupenda. Na haidhuru jinsi ulivyo, ningali nakupenda.”

¹³⁰ Siku chache baadaye, yeye alikuwa akila chakula chake cha mchana na wajoli wake kwenye chumba cha kuchemshia maji, alikuwa akiwasimulia hayo, kasema, “Naam, mtu angaliweza kutenda jambo baya vipi huku mtu fulani akupenda hivyo?” Mwaona?

¹³¹ Naam. Unge—ungevunjaje uaminifu huo?

¹³² Na tulipokuwa wenye dhambi, tumefarikishwa, bila Mungu; duniani, katika takataka za matope, kama nilivyonena asubuhi ya leo, Mungu akatujia! Mungu alikutafuta wewe, wewe haukumtafuta Mungu. “Hamna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Naye Mungu akashuka katika takataka hiyo, jinsi ulivyokuwa, na kukutafuta hata akakutoa! Hiyo inapaswa kuumba Upendo Mkamilifu. Tazama ulivyokuwa, na tazama ulivyo. Nini ilisababisha hilo? Mtu fulani aliyekupenda! Je, huwezi kuwa na imani katika yale aliyokuahidi, basi? Upendo halisi na dhahiri utaumba matumaini katika Neno Lake.

¹³³ Yeye alinipata nilipokuwa si kitu mimi. Ningali si kitu, bali nimo mikononi Mwake. Unaona, alinipata. Na alinipenda nilipokuwa sipendeki. Alikupenda ulipokuwa haupendeki, bali akakubadilisha. Kama tu yule Dada mweusi alivyosema, wakati ule katika ushuhuda wake, yeye alisema, “Mimi—mimi siko inipasavyo kuwa, siko jinsi ninavyotaka kuwa, bali siko jinsi nilivyokuwa!” Yeye alijua alifika mahali fulani, jambo fulani lilitendeka. Na hivyo ndivyo ilivyo. Mungu, nilipokuwa nimefarikishiwa Naye, alinipenda sana hata akainama chini kunishika na kuniinua, hilo linanipa matumaini kwamba Yeye anataka kunitumia. Yeye ana kusudi la kufanya hivyo. Aliona kitu fulani ndani yangu. Aliona kitu fulani ndani yako. Yeye alikuwa na sababu ya kukuokoa, watazame watu ambao hawajaokoka siku hizi. Watazame mamilioni ambao angaliwachukua akuache, bali alikuchukua. Amina! Hamna mtu anayeweza kupachukua mahali pako. Amina! Wewe umo katika uchumi wa Mungu. Hamna mtu anayeweza kufanya hivyo. Huo ni upendo Wake kwako.

¹³⁴ Basi je, upendo wako hauwezi kumfikia Yeye? Pia kuna mapenzi. Haidhuru jinsi hali ilivyo, hali ya mambo inaongozwa na Upendo huu unaumba Imani: ya kwamba Mungu anakupenda nawe wampenda Mungu, nanyi mnapendana, na—na hiyo inaleta Imani. Vema. Basi haiwezi... bali haiwezi kujizuia kutoa tu yale Mungu aliyoahidi itafanya.

¹³⁵ Basi, tazama! Imani iliyo Kamilifu ni safi, ni safi kama tu upendo ulivyo msafi. Waona? Basi, unapompenda mtu fulani, nawe una... unampenda bwana wako ama unampenda mke

wako. Naam, hamna haja kwa mtu ye yote kukwambia ya kwamba “hupendi,” kwa sababu unampenda, na unajua ya kwamba unampenda.

¹³⁶ Basi, kama ningaliuliza, “Wawezaje—wawezaje kuthibitisha ya kwamba unampenda?”

¹³⁷ “Lo, ninathibitisha hilo jinsi ninavyoishi kwake.” (unaona?) “Mimi ni mke wa kweli na mwaminifu. Mimi ni mume mwaminifu na wa haki, na hiyo inanithibitishia ya kwamba na—nampenda mke wangu; au nampenda mume wangu.” Waona, maisha yako yanathibitisha ulivyo. Ukristo hufanya jambo lile lile. Unaona? Imani yenu, mnaaminiana, ni safi. Na ni jambo halisi, ambalo hauwezi kulionyesha mtu mwingine, bali unalo, na matendo yako yanathibitisha hilo.

¹³⁸ Na unapopata Imani safi, isiyogoshiwa, kama upendo wako ulivyo kwa mwenzio, basi unaithibitisha kwa matendo yako. Haunung’uniki tena, unajua imetendeka, endelea tu kusonga mbele. Haidhuru jinsi mambo yalivyo, yale mtu ye yote asemayo, unajua ilivyotendeka. Unajua imekwisha; jinsi tu ujuavyo ya kwamba wampenda mume wako, jinsi tu vile ujuavyo unampenda... Unaona, upendo na imani havina budi kwenda pamoja. Ni jamaa moja, wanapendana. *Upendo huleta Imani.*

¹³⁹ Shetani anapotujaribu, inatupasa kumpinga kwa Imani Kamilifu katika Neno Kamilifu, kama Yesu alivyofanya. Neno la Mungu ni kamilifu. Inatupasa kuwa na Imani Kamilifu katika hili Neno Kamilifu, na kumpinga Shetani.

¹⁴⁰ Sasa, hebu tuharakishe, upesi tuwezavyo.

¹⁴¹ Kwa Imani Yake katika—katika Neno Lake (Yeye hushinda), tunaweza kushinda cho chote: mauti, kuzimu, na kaburi. Tunajua ya kwamba Mungu ni Mungu, ile Imani Kamilifu katika Neno Kamilifu la Mungu, Yeye alishinda kila kitu ambacho alikabiliana nacho. Hata mauti hayangalisimama mbele Zake. Magonjwa hayangalisimama mbele Zake. Kutoka kwake ilikuwa kama mito yenye nguvu, ikitiririka daima, nguvu zikitoka kwenye vazi Lake. Watu hawa, waliolala vivulini, waligusa tu vazi Lake nao wakaponywa. Yule mwanamke alipotenda hayo, ndipo kila mtu alitaka kugusa vazi Lake, kwa maana waliona ya kwamba alikuwa akitokwa na nguvu daima, zikitiririka kama mito. Alikuwa pale, akitembea, akitembea ulimwenguni na Imani Kamilifu, kwa sababu Yeye alikuwa Neno.

¹⁴² Na sasa, “Mkikaa ndani Yangu,” kupitia Kwake, Yeye alileta Neno kwenu; “na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu,” basi enendeni vivyo hivyo: nguvu zikitoka kwenu, mito ya visima vya baraka za Mungu ikiwatiririkia watu. Mnaona ninayomaanisha? Nawe hudanganyi, huwazii hayo. Inatendeka kweli, nawe unaiona. Iwapo unaiwazia tu, hilo halikufai kitu; bali iwapo iko, ilitendeka kweli.

143 Sasa tazama! Unaona, kwa hiyo, aliposimama na kusema, “Kama mkiuvunja Mwili huu (hili Hekalu), nitaufufua tena kwa siku tatu.” Kwani? Yeye alitosheka kabisa ya kwamba angalifanya hivyo, kwa maana Mandiko yalisema angefanya hivyo (yule Masihi): “Sitaiacha roho Yake katika kuzimu; wala sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Nabii, ambaye hujiliwa na Neno, alikuwa amesema hiyo ingetendeka, Naye alijua ya kwamba Yeye alikuwa Mtu huyo.

144 Na wakati. . . Yesu, Mwenyewe, kasema, “Na kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule,” ama “Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Kama. . .

Huna budi kuwa na matumaini yayo hayo makamilifu ya kwamba “nikiwekewa mikono, nitapata afya,” maana Yeye alisema hivyo.

145 Yeye alisema, “Uangamizeni Mwili Huu, Nami nitaufufua,” maana alijua Yeye alikuwa Masihi. “Sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu”; Yeye alijua alikuwa Yule Mtakatifu. “Wala sitaiacha roho Yake katika kuzimu”; Hakuiacha. Alijua atatenda hivyo. Yeye alikuwa na hakika ya kwamba alikuwa pale kushinda mauti na kuzimu, kasema, “Uangamizeni, mkitaka, nami nitaufufua tena kwa siku tatu.” Lo, jamani! “Ninao uweza wa kuutoa Uhai Wangu, nina uweza wa kuutwaa tena.” Yeye alijua alikuwa nani.

146 Wewe ni Mkristo. Una haki ya baraka yo yote ya wokovu ambayo Yesu alikufia wewe. Zote ni zako! Zimeisha lipiwa, inakupasa tu kuamini. Si kuwazia hayo; bali kuamini, na kujua ya kwamba ni zako, nawe unaweza kuzichukua. Lo, hiyo ndiyo Imani yenye kushinda: kujua! Hebu sisi. . .

147 Yeye alijua hapo mbele ingetendeka. Angebashiri kwamba ingetendeka, kwa maana alijua ingetendeka; na cho chote alichotabiri, kilitukia. Sasa, tazama! Cho chote alichosema, Mungu aliheshimu alichosema. Wazia hilo! Cho chote alichosema Yesu, Mungu alitimiza. Hivyo basi, alijua Maneno Yake yalikuwa Maneno ya Mungu. Sasa tazama! Andiko lilo hilo linaturudia sisi moja kwa moja tena, “*Ninyi* mkiuambia mlima huu.” Lo, jamani! Ni—nitaacha hilo lingie ndani kidogo, mwaona, maana tutafanya mstari wa maombi. Tutaliachilia kusanyiko lipumukane na kuwaombea wagonjwa, wale wanaotaka kuo. . . ambao hawana budi kuondoka.

148 Tazama! Yeye alijua ya kwamba alimpendeza Mungu. Alijua ya kwamba hamna neno juu ya maisha Yake. Mungu tayari alikuwa ameshuhudia ya kwamba, “Huyu Mwanangu, mpendwa Wangu, nimependezewa, msikieni Yeye! Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake,” katika siku ya ubatizo Wake. “Nimependezwa kufanya maskani Yangu humu, hamna hukumu ya dhambi Kwake kamwe.”

¹⁴⁹ Sasa, wakati Mungu yule yule anapokuja kwako, na apendeze kukaa ndani Yako, akapendeze kuheshimu neno lako, maamuzi yako, . . . Maamuzi ya Yoshua yalikuwa nini? “Simama kimya, jua!” Nalo likasimama pale. Amina! Bila shaka! Je, maamuzi ya Musa yalikuwa nini? Akainua kijiti chake juu—juu ya mto *hivyo*, kisha akauamuru “ugawanyike!” Nao ukagawanyika! Unaona, ni lo lote uombalo. “Nawe ukivambia mlima huu, ‘Ondoka,’ na usione shaka” (waona, moyoni wako) “ila uamini kwamba hayo usemayo yametukia, yatakuwa yako (yale uliyosema).” Hiyo inakurudisha *wewe* katika Neno. Naam, hayo si maziwa ya mtindi. Inakurudisha *wewe*. Ninajua itawapitia juu hapa, mwaona, kwa maana haiwezi kutia nanga; bali imani halisi na ya kweli itashika hayo, sasa hivi.

¹⁵⁰ Nimeiona, rafiki. Iko hapa hii Biblia ikifunguliwa mbele zangu. Nimeiona ikitendeka, nami najua ni Kweli. Najua, Mungu aliye Mbinguni anajua, ya kwamba huenda nisiishi nikamalize ujumbe huu, bali na—najua ya kwamba ilitendeka. Nimeiona mimi binafsi. Mimi ni shahidi wa Neno hilo likitimizwa, nami najua ya kwamba ni Kweli: nikanena, na kusimama pale na kuona Muumba akiumba kiumbe kilicho hai, mbele ya macho yangu kabisa; unaendelea kutikisa kichwa chako na kushangaa; kisha kuangalia humu na kumwona Yeye akileta mwingine, anayefanana kabisa na yule mwingine, kwa maana *wewe* ulisema hivyo; na kusonga huku na kusema, “Kutakuweko na mwingine pale,” na kutazama, ndiye huyo! Sasa, hiyo ni kweli.

¹⁵¹ Jamani, tunapaswa kuwa wapi? Hiyo ndiyo Imani Kamilifu. Hamna ono, “Nena tu Neno”, sikuona kuchakulo kamwe. Yeye alisema tu Andiko *hili*, jinsi lilivyokuwa, na “Linene, na usione shaka; bali usemalo, litatimia.” Nami nikaamini Neno la Mungu, nalo likatimia. Hiyo ni kweli. Hiyo ina nguvu tu. . . Basi rafiki, kama mchungaji wako, hilo lina nguvu tu kama lilivyokuwa wakati Yoshua alipolisimamisha jua; kwa maana jua lilikuwako tayari, kitu hicho kilikuwa kikienda, naye akakomesha huo mwendo. Bali hili, yeye alileta kitu hapo ambacho hakikuweko, Yeye akaumba!! Mimi nina furaha sana kujuana na Mungu ambaye anaweza kuchukua haya mavumbi ya ardhi, siku moja bila cho chote, na kunifufua tena baada ya kuzikwa kaburini. Lo, jamani! Ndiyo hiyo:

Imani Yangu inakutumainia,
Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,

¹⁵² Unalisema na usione shaka, bali uamini uliyosema, yatakuwa yako. Unaona, amini ya kwamba itatendeka!

¹⁵³ Daudi, katika Zaburi, alinena habari Zake. Na kwake, Yeye akachukua uweza Wake na kuwahudumia wengine. Hakuuweka Kwake tu, bali alihudumia Wengine kwake; pia akawaokoa wengine, kabisa. Naye anaweza kufanya jambo lile lile sasa. Na aliwaahidia waamini jambo lile lile katika Neno Lake, na

Yohana . . . kama Yohana 14:12, Yeye alisema hivyo; Marko 16; na pia katika Marko 11:23, ambapo tumesoma.

¹⁵⁴ Naam, tazama. Sasa, ameonekana kwetu katika umbo lile lile aliloonekana kwao katika Agano la Kale, na kama vile alivyofanya katika Agano Jipya; Naye ameonyeshwa kwa Neno lile lile, Kristo yule yule. Nami nawatangazieni ya kwamba Kristo ndiye Roho Mtakatifu. Ne—neno *Kristo* maana yake ni “mtiwa mafuta”; mtu tu aliyetiwa mafuta, huyo ndiye Kristo, aliyetiwa mafuta. Wangapi wanajua ya kwamba hiyo ni kweli? Aliyetiwa mafuta, kungekuwa mtu ambaye ametiwa mafuta. Ametiwa mafuta na nini? Biblia ilisema katika Matendo 2, ya kwamba Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa na Mungu, akatiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu; akazunguka huko na huko na kutenda kazi kuu na kadhalika, waona, ambaye Mungu alidhihirisha, na kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndani ya mtu huyo.

¹⁵⁵ Na sasa, tunakuwa watiwa mafuta kwa Roho yuyo huyo, masihi watiwa mafuta, masihi wa siku za mwisho, kuangaza ufufuo wa Yesu Kristo; kuonyesha ya kwamba si mfu, bali yuko katika umbo la Roho Mtakatifu, yu ndani ya watu Wake, akitembea kati ya Bibi-arusi Wake, akimfanyia mapenzi, akijimwaga Mwenyewe Kwake. Wanakuwa mmoja kwa ajili ya Karamu ya Arusi; na ishara zile zile, zilizoahidiwa na Mungu yule yule, katika Neno lile lile zinafanya madhihirisho yale yale Yake.

¹⁵⁶ Hamna kilichobaki kwetu ila kuliadini, na “kuliadini” ndiyo *hakika ya mambo*, na hiyo huumba Imani Kamilifu. Waza tu jinsi—jinsi tulivyo walegevu; waza hilo tu kwa muda mchache, sasa.

Naam, hebu tuone:

¹⁵⁷ Je, ametenda mambo yote vizuri? Je, ametwambia lo lote kamwe, ila lililotendeka hasa jinsi Yeye alivyosema? Je, Yeye hajafanya, na je, ile Nguzo ya Moto iliyo kuu haijakuwa miongoni mwetu na kufanya hasa kama alivyoahidi kufanya? Je, hatujaiona? Si sayansi imeipiga picha, baada ya kubashiriwa yatakayotendeka; ikapelekwa kule na kuchapishwa kwenye magazeti ya kila siku na ya mara kwa mara, yakaichapisha na kuonyesha, na huku mliambiwa hayo miezi kadha kabla haijatendeka? Je, si Yeye ametenda vile vile hasa alivyotenda katika Agano la Kale, na Agano Jipya? Na ni yule yule Mmoja hasa! Roho Mtakatifu yule yule yuaja, naye ni mtambuzi; nalo Neno la Mungu, ambalo ni jepesi, tena lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, linalotambua mawazo na maksudi ya moyo. Sivyo? Si huyo ni Mungu yule yule? Na Yeye ni Mtu yuyo huyo, si mgeni huko mahali pengine, Yeye yuko hapa. Yeye yuko hapa, anatenda haya kuumba Imani Kamilifu. Ninamsikia. Najua Yeye yuko hapa sasa. Najua ya kwamba Roho Wake yuko hapa. Najua

ya kwamba Yeye anajua mambo yote. Amina! Nami najua Yeye anataka ku—kufanya jambo fulani. Amekuwa akifanya jambo fulani, ku—kuumba huu ukamilifu wa imani katika watu.

¹⁵⁸ Je, tutaingia katika Umilele, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na nafsi nane zilizookolewa? Tutakuja kama Lutu, na watatu kutoka Sodoma? Je, tutakuja, kama siku za Yohana Mbatizaji, na waamini sita? Hebu na tuamini, kwa maana kazi Zake ni kamilifu! Zinadhihirishwa kila siku na kikamilifu mbele zetu, zikionyesha ya kwamba Yeye ni Neno, Neno! Waebrania, sura ya 4, inasema:

... neno la Mungu li... lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, ... hata kuyatambua mawazo na maksudi ya moyo.

¹⁵⁹ Wazia hilo! Neno la Mungu ndilo *Hilo*, mtambuzi wa maksudi ya moyo. Maana Neno la Mungu li jepesi, tena lina nguvu, na lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena linayatambua mawazo na maksudi ya moyo. Neno lililofanyika mwili! Haleluya! Neno likitenda kazi katika mwili wa mwanadamu, kwa ishara za kimwili kwa ishara za vitu, kwa ishara za Kimaandiko, kikamilifu, kuwaleteeni Imani Kamilifu kwa ajili ya Kunyakuliwa Kukamilifu.

¹⁶⁰ Mbona hatuwezi kuiangalia? Si fumbo; Shetani ameweka kila kitu duniani mbele yako, kujaribu kukuweka—kukufanya—kukufanya usiliamini. Ataleta mkutanoni na kujaribu kutupilia cho chote awezacho mbele yako. Kuiondoa kwako! Biblia inasema, “Inuka, ukajitikise.” Kaa chonjo.

¹⁶¹ Roho Wake yuko hapa, Yeye anakujua. Inakupasa kufanya jambo moja, na hilo ni kumuamini, kumpokea. Yeye anakujua. Je, unaamini hilo? Anajua kile kilicho ndani yako, anajua wewe u nani, anajua haja zako, anajua mahitaji yako.

¹⁶² Jim, unaamini ya kwamba Yeye anajua habari za huyo mtoto mchanga? Aliugua homa kabla hujaondoka, kipimo cha joto mia na tano. Je, unaamini Yeye atamponya? Ulimshika leo, huo ugonjwa, “Utamwacha.” Nalitazama tu kule na kuwaona kabla hawajaondoka nyumbani, waliyotenda. Sasa, hiyo ni kweli.

¹⁶³ Bi. Little, je, unaamini ya kwamba Mungu atakupa ushindi juu ya huo ugonjwa wa sukari? Kuna mwanamke anayeketi kando yako, sikujui, bali Roho yuko juu yake. Kinachomfadhisha ni mtoto...yuna mtoto mdogo anayetakiwa kufanyiwa upasuaji wa jicho ama kitu fulani. Ametoka Chicago. “Jepesi, lina nguvu, kuliko upanga ukatao kuwili; huyatambua.” Ni nini? Neno! Mnaamini hilo? Bila shaka.

¹⁶⁴ Kuna bibi anayeketi papo hapo kwenye hiyo safu nyingine; umeishafanyiwa tu upasuaji wa jicho, haukufaulu sana. Bali una—unaamini, litapata...uta—utapata afya. Unaamini? Vema, umeponywa. Ulikuwa ukiwazia hayo.

165 Bi. Peckenpough, si kwa ajili yako, ni kwa ajili ya huyu mjukuu anayeketi hapa. Unaombea hilo, bali unaamini ya kwamba Mungu atakupa afya? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia kilicho kasoro. Madaktari hawajui; la. Hiyo ni kweli. Mapafu yanayovimba. Hiyo ni kweli. Yuna ugonjwa wa damu. Hiyo ni kweli! Umetatizika kama utamwacha aende shuleni ama sivyo. “Jepesi, tena lina nguvu, kuliko upanga ukatao kuwili.”

166 Namwona mwanamke akipoteza chakula chake. Yeye yuko mahali fulani, hebu nipate uso wake mahali fulani. Naam anaketi nyuma. Jina lake ni Bi. LewEllen. Yeye anaamini kwa moyo wake wote, huo ugonjwa wa tumbo utakuacha. Amina!

167 Hapa mna bibi anayeketi upande ule mwingine toka kwake, anayenitazama sasa hivi, ameketi hapo mwisho; amevalia miwani. Yuna yabisi kavu. Iko katika mkono wako wa kushoto; ilikuwa huko, haiko sasa. Ni ukiamini tu!

168 Na je, huyo mtoto mchanga, kule nyuma kabisa? Ametoka Ohio; yuna kansa jichoni mwake. Je, unaamini ya kwamba Mungu atamponya? Atafanya hivyo, wewe amini. Ashland, Ohio! Amini sasa ya kwamba Mungu atakuponya, Naye atafanya hivyo. Ni nani? “Lina nguvu, ni jepesi kuliko. . .”

169 Hapa yuaketi bibi, kitu fulani kilimgusa, ana mauvivu begani. Hiyo ni kweli. Sivyo? Vema, amini, na yatakuondokea, Unaona? “Neno la Mungu, huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.”

170 Naam, hamna kadi za maombi katika jengo hili. Hamna mtu wa kuombea. . . kusambasa kadi za maombi. Hatuzitumii humu, hizo ni kwa kuweka utaratibu tu. Unataka kuombewa? Ni wangapi wanataka kuombewa wakati Neno linapodhihirishwa katika mwili? Hebu safu hii hapa isimame ije upande huu, moja kwa moja kupitia marefu haya hapa kwanza, papa hapa, ninyi mnaotaka kuombewa. Kisha, baada ya hayo, nataka marefu haya hapa yawafuate. Kisha baada ya hao kumalizika, hebu na marefu haya humu yaje.

171 “Jepesi, tena lina nguvu. . .” Je, upanga ukatao kuwili waweza kufanya hivyo? La, bwana! Bali Neno la Mungu linaweza kufanya hivyo. Kwa nini? Ni Neno la Mungu. Basi, mnaamini?

172 *Ni Tabibu wa Karibu!* Yuko wapi yule Dada kutoka kule—kule Tennessee, Dada Ungren. . . Downing? *Ni Tabibu wa Karibu.*

173 Sitasahau hayo, kule Fort Wayne usiku huo wakati yule maskini msichana wa Kiamishi ama Dunkard alipokuwa ameketi pale, na kucheza, *Ni Tabibu wa Karibu*; aliposikia ya kwamba huyo mvulana mdogo aliponywa, aliruka juu, Roho Mtakatifu akashuka juu yake, nywele zake nzuri zikamfunika mabegani, na hicho kinanda hakikukosa huo wimbo. “*Ni Tabibu*

wa Karibu, Tabibu wa ajabu.” Nguvu za Kimbinguni zikicheza hicho kinanda, kikiimba “*Ni Tabibu wa Karibu.*”

¹⁷⁴ Tazama, je... Unaamini? Inakupasa kuamini? Sasa kumbuka, unapopitia... Sasa, kama huamini, usije, keti chini. Kaseme, “Mimi... Sita sitawakwaza hawa hapa. Ninakuja nikiamini.” Wakati mimi...

¹⁷⁵ Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Hiyo ni kweli hasa. Basi, hiyo ni chini ya masharti, “kama unaamini.” Sasa, naamini Mungu amewathibilishia naamini. Mnaona? Yeye hudhihirisha Neno Lake, kuonyesha ya kwamba ni Neno Lake. Timilizo la Andiko, kuthibitisha ya kwamba ndivyo ilivyo. Naam, wewe amini unapopitia hapa. Mtafanya hivyo? Kisha nikiweka mikono juu yenu, ... hivyo ndivyo hasa Biblia ilivyosema.

¹⁷⁶ Je, una mafuta ya kupaka hapa, Ndugu Neville? Yachukue, na uje upande huu, hebu tu tutimize Maandiko. Kuja upande huu hapa, na umpake mafuta kila mtu anayepita na tutawaombea. Sasa, ili nipate kujua ya kwamba nitapata kuomba kwa imani kwa ajili ya kila mmoja wenu, hebu kila mtu mkawekeleane mikono yenu ninyi kwa ninyi mlio waamini. Nyosheni na kupishiana mikono ninyi kwa ninyi. Hapa ndipo tutakapopata kitu fulani kwa dakika chache.

¹⁷⁷ Nitaona jinsi kanisa langu limeendelea mbele kwa yale tunayoamini, mwaona. Kuona vile watu wameendelea mbele; jinsi walivyo tayari kuchukua Upanga na kuingia mstari wa mbele, kaseme, “Nakuhimiza, Shetani. Nakuhimiza! Huwezi—hauwezi kunifanya nisiamini tena!” Kwa nini mambo haya yanatendwa? Kusudi watu wapate kuamini. Ni Neno. Ni hapo ambapo hiyo inaonyesha ya kwamba ninawahubirieni Ukweli, Neno. Neno lililofanyika mwili, lililofanyika mwili ndani yenu; lililofanyika Neno, lililofanyika Uzima ndani yenu, lililofanyika Uzima ndani yangu. Mwaona?

Ni Tabibu! Vema, hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa:

¹⁷⁸ Bwana Yesu, yule Tabibu Mkuu sasa yu Karibu, Wewe ndiwe Tabibu. Nimehubiri Neno Lako, nalo Neno Lako limetangaza ya kwamba Wewe uko hapa; ya kwamba ni Wewe yule jana, leo, na hata milele; ya kwamba hauwezi kushindwa. Haujapata kutupungukia, Bwana. Na sasa, hebu kila mmoja wa hawa waliowekeana mikono, na baraka za Mungu ziwe juu yao. Na tunapokuja nao ni waamini, na tunapowapaka mafuta, mchungaji pamoja nami, na ninapowapisha katika mstari huu, na kila mmoja apitie hapa akiwa na imani ya kuamini, na kujua ya kwamba Mungu yule yule wa Mbinguni anasimama hapa. Na kila mmoja wao ajitikise. Je, wanaweza mara hii moja tu, Bwana? Hebu tu wao... hebu na iingie ndani, Bwana, mara moja zaidi. Yafungue macho yao, Bwana, wapate kuona yanayoendelea, na

wasiwe vipofu, wakiyumbayumba bali kuona ukweli wa Uwepo wa Yesu Kristo aliyefufuka. Tujalie, Bwana, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁷⁹ Nakuagizeni katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba usije kwenye mstari huu isipokuwa unasikia ya kwamba una Imani Kamilifu, maana unapoteza tu wakati wao, wakati wa mtu mwingine. Usifanye hivyo! Na kwa... tangu nilipoanza kuwahubiria, je, nimesema kamwe neno moja kwenu isipokuwa lile lililotendeka? Vivyo hivyo! Bwana alitenda hayo. Hakufanya hivyo kwa ajili yangu, naamini. Alifanya hivyo kwa ajili yenu, mpate kuamini ya kwamba ninayowaambia ni Kweli. Sasa aminini, itakuwa sawa, na ita... utapata afya. Unapopitia hapa, tumbukiza kutokuamini kwako papa hapa katika huu... mfuko wa Kiroho hapa. Hautauona, bali uko. Mafuta hayo yatakapokugusa, tumbukiza kutokuamini kwako humo. Kuweke humo na uende zako ukiwa na Imani Kamilifu ya kwamba umepata afya. Je, utafanya hivyo? Bwana akubariki basi.

¹⁸⁰ Vema, nitamuuliza mtu fulani anayeweza kuongoza nyimbo, ku... Yuko wapi yule mhubiri mashuhuri, ndugu, ambaye...? Jina lake ni nani? Capps, Ndugu Capps. Yuko mstarini? Ati nini? Njoo hapa, Ndugu Capps, ukasimame pale uimbe (kusanyiko) sote tunapoomba, *Ni Tabibu wa Karibu*, huku wao—wao... kila mmoja akiimba sasa, kwa moyo wako. Usiimbe tu, ukisema, “Nitaimba: ni, tabibu, wa, karibu, tabibu wa ajabu na rehema za daima, tabibu wa ajabu.” Lo, lo, jamani!

Shikeni zamu, mkiwa mnasimama, mkiwa macho: “*Naam, ni Tabibu wa Karibu, Tabibu wa Ajabu.*” Anathibitisha ya kwamba Yeye yuko hapa! Namwamini Yeye. Amina.

¹⁸¹ Vema, hebu... hebu wale walio na imani waje mbele. Katika Jina la Yesu Kristo, namwekea mikono dada huyu kwa uponyaji wake. [Ndugu Branham anaomba wagonjwa—Mh.]... Wote wamekwisha?

¹⁸² Sasa, hebu tuinamisheni vichwa vyetu sasa:

Ni Tabibu wa Karibu;
Tabibu wa ajabu;
Na rehema za daima;
Ni dawa yake njema.

Imbeni, malaika,
Sifa za Yesu Bwana;
Pweke limetukuka
Jina Lake Yesu.

¹⁸³ Je, mumeelewa na hayo niliyowatendea? Ninyi mumeniita “mchungaji wenu”; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Ikiwa mimi, niliye mchungaji wenu, nimekwisha tambulishwa na Yesu Kristo, ya kwamba mimi ninatenda kazi Yake, basi aminini Neno langu. Kwa kutenda hili tendo la imani, kwa kuweka mikono yangu juu yenu, nimekwisha kuhukumu

magonjwa na mateso yanayowasumbua. Aminini hayo, ndipo mtatimiziwa haja zenu, hata ziwe ni nini, kwa maana mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio. Na mnapoomba, aminini ya kwamba mmepokea mlichoomba. Nami naamini kabisa ya kwamba napokea, na moyoni mwangu napokea uponyaji wa kila mmoja wenu, naupokea, ya kwamba umetendeka. Naamini, naamini hayo kwa yote yaliyo ndani yangu. Pia, huku mikono yangu ikiwa juu ya vitambaa hivi vilivyo hapa, nimekuwa nikiviangalia kwa makini, naamini ya kwamba vitatoa yale hasa watu waliyoomba. Na—naamini hivyo.

¹⁸⁴ Hii inaelekea kwenye ule Mvuto wa Tatu! Ni—ninaamini hilo. Sasa nataka kuwaulizeni swali la moyoni, ninyi mliopitia kwenye mstari wa maombi. Mnaweza kuamini kweli, na kujisikia sasa, ya kwamba mna jambo lililotendeka ndani yenu tangu mlipowekelewa mikono? Vema; inueni mikono yenu. Ndilo hilo. Hili ndilo tumekuwa tuingojea. Naam, hili si... hili linaanza tu kuchanua sasa. Mwaona? Limeanza na... Nilifanya hili kwa kusudi fulani. Nilifanya hili kwa kusudi fulani. Ninafanya jambo fulani, ni kuchukua agizo hili la imani na kurudi kule nyuma kuanzia halafu kuingia; mwaona, nipate kuinua imani kufikia kiwango ambacho hamjaiona hivyo hapo mbeleni. Si imani, bali Imani Kamilifu, iliyojengwa ndani humu. Na kumtazama Mungu aliye mkamilifu, kwa moyo mtimilifu, akitimiza ahadi kamilifu, kwa Neno Lake lililo kamilifu, ambalo lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili na huyatambua mawazo yaliyo moyoni. Kwani? Tunakaribia sasa ule ukamilifu, kwa maana watu hawana budi kuufikia kwa ajili ya Kunyakuliwa. Hiyo ndiyo inayozuia sasa hivi, ni kungojea hilo Kanisa lifikie hiyo Imani Kamilifu ya Kunyakuliwa. Ninaitazamia. Inamaanisha kufinyangwa sana kwangu mimi, ni muhimu sana kwenu, bali sote pamoja tutafaulu kwa Neema ya Mungu. Amina.

Ni Tabibu wa Karibu;

Tabibu wa ajabu; (Bwana Yesu, mpe ndugu huyu mpenzi... Na Roho Wako Mtakatifu daima ampe mchungaji huyu afya; na kumhifadhi, ali mwenye afya na mwenye nguvu, safarini mwake hata utakapomwita. Katika Jina la Yesu. Ninadai hayo, Bwana, nampenda. Sisi wote wawili tunadai hayo, nasi sote wawili tuna imani...?)

Na rehema za daima,

Ni dawa yake Nyena.

¹⁸⁵ Je hamumpendi? Waza tu: papa hapa sasa, ameisha anza kazi ndani ya mwili wako, ya kuponywa kwako, kwa maana Yeye aliahidi itatendeka. Na sasa (mnaona?), mlishika niliyokuwa nikisema usiku wa leo? Mmefahamu mafumbo yake? Unaona, “Kama wewe ukiuambia mlima huu,” usione shaka, usione shaka

bali uamini uliyosema. Sasa tazama, katika muda wa chini ya dakika tano, kila mkono uliinuliwa ya kwamba kazi imekwisha kuanzishwa ndani yao sasa hivi. Lo, jamani! Ndiye huyo. Ndiyo hiyo! Ni nini? Uwepo wa Tabibu wa Karibu.

¹⁸⁶ Lo hebu tuinue mikono yetu kwa Mungu na kuuimba tena:

Ni Tabibu wa Karibu;
Tabibu wa ajabu;
Na rehema za daima;
Ni dawa yake jema.

Imbeni, malaika,
Sifa za Yesu Bwana;
Pweke limetukuka
Jina Lake Yesu.

¹⁸⁷ Hebu na tusimame kimya kwa dakika moja. Hebu na tumwabudu tu mioyoni mwetu. Wazia hilo: Koma, Yeye yuko hapa. Yuko hapa. Nani? Nani alijitambulisha kuwa Neno? “Hapo mwanzo alikuwako Neno, Naye Neno alikuwa kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, Yeye yule jana, leo, na hata milele. Neno lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, hata huyatambua mawazo na makusudi (kilichokuleta hapa, kusudi lako la kuwa hapa, wewe u nani)”; likamtambulisha Yesu Kristo kuwa Masihi, na leo linamtambulisha Yeye kuwa Masihi yule yule jana, leo, na hata milele.

¹⁸⁸ Tabibu wa Karibu Aliye hapa, Ambaye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya. Na ukivambia mlima huu, ‘Ondoka,’ na usione shaka moyoni mwako, bali waweza kuamini kwamba Yeye aweza kuumba kuchakulo,” ambao hawana njia kamwe, ama hamna kitu cha kuaminia; ni imani yangu ambayo inaenda na kutenda hayo, imani yangu kwa yale aliyonihimiza kuomba. Alinihimiza kuomba. Nami nikapokea himizo Lake kwa kutii Neno Lake, niliomba, na ikatendeka! Mungu aliye Mbinguni ajua hilo ni kweli. Je, anaweza pia kuponya wagonjwa? Iwapo anaweza kuniinua kwa imani hivi, hata kwa ajili ya watu, hata ingawa hawezi kupanda kufikia kile kiwango. Ona? Iwapo wao hawawezi kufanya hivyo, Yeye anaweza kutumia imani yangu. Anaweza kuniinua hata mahali hapo, nami napanda huko kwa ajili yenu. Ninaamini kwa ajili yenu. Ninanena kwa ajili yenu.

¹⁸⁹ Mimi ni ndugu yenu, nasimama kama ndugu yenu mwombezi, nikijaribu niwezavyo kuwaweka mbele za Mungu. Nami nasimama hapa mbele ya kile Kiti Cheupe cha Enzi sasa, nikichukua ile... nikielekezea kidole changu kwenye ile dhabihu iliyolowa damu pale, na kusema katika Jina Lake ya kwamba imetendeka. Haina budi kutendeka, na haina budi kutendeka. Unajua imetendeka. Ninajua imetendeka, pia wajua imetendeka, na ndivyo ilivyo. Hiyo ni Kweli. Amina.

...limetukuka
 Jina Lake Yesu.
 Imbeni, malaika
 Sifa za Yesu Bwana;
 Pweke limetukuka
 Jina Lake Yesu.

¹⁹⁰ Na pepo walikuwa wanatutii sisi katika Jina Lako, Jina lililo tamu sana katika ulimi wa mwanadamu. Pepo...A—Ambalo huwafufua wafu, Ambalo huwaponya wagonjwa, Ambalo huwatakaswa wenye ukoma, Ambalo huwatoa pepo, Ambalo huwafanya Wakristo. Hamna Jina jingine chini ya Mbingu. Mimi huishi ndani Yake, nimebatizwa Kwake, nimeliamini, huabudu Kwalo. Lo, hebu niwe sehemu Yake. Hebu nipoteze utu wangu; kisha nilipate, Bwana, Kwako, hilo Jina liitwalo Yesu Kristo, Masihi mtiwa mafuta, nipate kujitahidi nitoke kwenye matope ya kutokuamini nipate kuonyesha uzuri wa Yesu Kristo: yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁹¹ Mungu awabariki sasa. Mtakaporudi hapa Jumapili ijayo, toeni ushuhuda wa jinsi mlivyoponywa, yaliyotendeka juma hili. Angalieni mwone kitendekacho. Imekwisha! “Wajuaje?”

¹⁹² Yeye aliniambia “sema,” nami nikasema. Imekwisha, sasa, imekwisha. Imekwisha. Naamini hivyo. Sasa, mchungaji, Ndugu Neville.

¹⁹³ Hebu kidogo. [Ujumbe katika lugha mpya, na tafsiri, kutoka kwa kusanyiko—Mh.] Jina la Bwana libarikiwe. Na tuinue mikono yetu tukamwabudu kwa muda mdogo. [Kusanyiko linaabudu—Mh.] Sasa, kama mwamini, je, uliona urefu wa ujumbe ulionenwa; na ulinganifu wake wa sauti, na kutazama tafsiri ikirudia yale yale. Ndivyo ilivyo. Tazama ulivyokuwa, uliambatana kabisa na Ujumbe; ikithibitisha ya kwamba kitu hicho kilikuwa Kweli, ya kwamba tayari Yeye aliisha tenda yale aliyoahidi kutenda. Tazama jinsi huo ulivyotoka, na tazama jinsi ulivyotafsiriwa. Tazama ni muda gani *yeye* alinena, na tazama ni maneno mangapi *yeye* aliyosema; vivyo hivyo hasa.

Bwana awabariki, hata nitakapowaona tena.



IMANI KAMILIFU SWA63-0825E

(Perfect Faith)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Agosti 25, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org